
SUPA JACKPOT
TZS. 1,065,505,647
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**MKURUGENZI** aingia matatani tuhuma kuuza viwanja viwili kwa Sh. bilioni moja




UKURASA 11

# Nipashe

Jumamosi Januari 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581190

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# MVUA KUBWA YA USIKU ILIVYOIBUA MAFURIKO

**FAMILIA** zakosa makazi, mahitaji... *Endelea uk.2*



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Mkoa wa Morogoro, wakifanya uokoaji katika kata ya Kihonda, baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko yaliyozizingira nyumba za wananchi, katika Manispaa ya Morogoro jana. Picha nyingine: Nyumba zikiwa zimezingirwa na maji. **PICHA: ASHTON BALAIGWA/IDDA MUSHI**

## ACT yaibwaga CUF kortini, kulipa fidia ya mamilioni

UKURASA 3

# Mahakama yatoa onyo kesi Mfalme Zumaridi

UKURASA 2

**MICHEZO** **IHEFU YAIREJESHA YANGA DARASANI** UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Mbunge wa Jimbo la Morogoro mjini, AbdulAziz Abood (aliyeshika fimbo), akiangalia baadhi ya nyumba zilizoharibiwa na mafuriko ya mvua katika kata ya Kihonda, jimboni humo jana. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Mvua ilivyoibua mafuriko usiku

**Na Waandishi Wetu**

MVUA iliyonyesha kwa zaidi ya saa saba mfululizo katika maeneo mbalimbali ya mji wa Morogoro, imesababisha watu kukosa mahali pa kuishi, nyumba na kuta kubomoka na kuzolewa na maji.

Sambamba na maafa hayo, pia watu wameshindwa kuvuka upande mmoja kwenda mwingine na kukwama kwa shughuli za uzalishaji mali.

Mvua hiyo imeathiri zaidi maeneo ya kata za Kihonda, Mkundi, Lukobe na Tungi, Kikosi Cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kimelazimika kuingilia kati kuokoa maisha ya watu na mali zao. Mvua hiyo ilianza kunyesha majira ya saa 6:00 usiku hadi jana saa 1:00 asubuhi.

Baadhi ya wananchi waliopata athari ya mafuriko wakiwamo Mgaya Ramadhani mkazi wa Mtaa wa Maelewano na Simon Mkude mkazi wa mtaa wa Magunila, walisema sababu kubwa ya mafuriko hayo ni uwapo wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kwa kuwa wananchi hawakushirikishwa kutoa ushauri katika ujenzi wa madaraja ili waonyeshe mikondo ya asili.

Kutokana na mafuriko hayo, waliiomba serikali iwasaidie kudhibiti mafuriko hayo ya mara kwa mara na kuwasaidia waathirika, hususani waliokosa mahali pa kuishi kutokana na nyumba zao kubomoka na hata waliopoteza mali vikiwemo vyakula na vyombo.

Mkude alisema tangu usiku saa 9:00 hawajalala kwa kuhangaika kutoa tope liliolingia na maji kwenye nyumba yake na kwamba vyombo vyote na vyakula vilionďoka na maji katika maeneo yao ya Mbuyuni, Majengo Mapya.

"Tulisikia mvua kubwa imeanza kunyesha kuanzia saa 8:00 usiku tukadhani ni mvua za kawaida, hivyo kuendelea kulala lakini baadaye nikahisi maji yanaingia ndani na nilipoamka nikakuta kweli yameingia, hivyo kuwaamsha mke wangu na watoto tutoke nje," alisema Mkude.

Alisema kazi waliyoifanya ni kuanza kutoa maji na tope. Aliiomba serikali kuangalia taratibu za kusaidia wananchi wake, huku akilalamikia ujenzi wa reli ya SGR kuleta athari zote kwenye makazi ya wananchi.

Mwathirika mwingine, Mwantumu Salumu, alisema wakati mvua inaanza, walishitukia maji yakiingia ndani na kusomba baadhi ya vitu. Alisema kwa sasa anahitaji msaada wa makazi na mahitaji ya chakula na kuiomba serikali kumsaidia kwa kuwa amepoteza kila kitu.

Mgaya Ramadhani mkazi wa mtaa wa Tuelewane, alisema miaka ya nyuma kabla ya Ujenzi wa SGR , mvua hazikuwahi kuleta madhara makubwa kama sasa kwa kuwa mikondo ya maji ilifuata njia zake tofauti na sasa.

Kaimu Kamanda Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Mkaguzi Emmanuel Ochieng, alisema watu 48 wameokolewa kutokana na athari hizo za mafuriko na wamehifadhiwa katika ofisi ya kata ya Kihonda kwa hatua zaidi.

Akiwa eneo la tukio, Ochieng alisema walipata taarifa ya athari hizo za mafuriko kutoka maeneo mbalimbali ya manispaa ya Morogoro na kwenda kuokoa ingawa hakukuwa na taarifa zozote za kifo wala majeruhi hadi jana jioni.

Kutokana na mafuriko hayo, aliwatahadharisha wananchi hususani walio kwenye mikondo ya maji na maeneo hatarishi, kuondoka maeneo hayo au kutafuta taratibu zingine salama kwa usalama wao na mali zao kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Na watu waliochimba mashimo ya taka na karo na kuyaacha wazi ni vyema wakafukia mara moja kwani ni hatari hasa kwa watoto na wazee," alisema Ochieng.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando amesema tayari ameitisha kikao cha kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ili kufanya tathimini ya athari iliyotokea na kwamba hadi wakati anazungumza alisema hakuna taarifa yoyote ya watu kujeruhiwa au kupoteza maisha.

Mkuu huyo wa wilaya pia alisema katika maeneo ya shule ambazo ziko kwenye maeneo hatarishi, walimu wakuu na wakuu wa shule wameagizwa kuzifunga kwa muda hadi watakapoona kuna hali ya usalama.

"Tunawaasa wananchi waendelee kuchukua tahadhari ya mvua kwani bado zinaendelea kunyesha na watoe taarifa kwa haraka pindi watakapoona tatizo lolote limejitokeza katika maeneo yao," alisema Msando.

Jana asubuhi, kutokana na mvua hizo, barabara ya Dodoma-Morogoro, eneo la Kihonda, ilifungwa kwa saa kadhaa kutoka majira ya alfajiri kutokana na kujaa maji ambayo mengi yanatokea milimani hata kama mvua zikiwa zimepungua na kuzidi kusababisha athari

Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, alisema kutokana na mvua hiyo, hali imekuwa mbaya na mafuriko yamekuwa mengi, hivyo kusababisha wananchi wengi kuathirika kutokana na baadhi ya nyumba kubomoka.

"Lakini tunashukuru Mungu wananchi wako salama na kwa kushirikiana na serikali ya wilaya hali imeendelea kuwa shwari," alisema.

Diwani wa Kihonda, Hamisi Kilongo, ambaye mitaa mingi katika kata yake imeathiriwa, alisema kunahitajika vyakula na makazi ya muda kwa walioathirika na mafuriko hayo.

• **Imeandikwa na Idda Mushi na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

## Mahakama yaonya ucheleweshaji upelelezi kesi Mfalme Zumaridi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza imeonyesha kutokuridhishwa na mwenendo wa waendesha mashtaka kwa kuchelewesha upelelezi wa kesi namba 11/2022 inayomkabili Diana Bundala, maarufu Mfalme Zumaridi.

Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Amani Sumari alibainisha hayo jana wakati akisikiliza kesi hiyo kwa niaba Hakimu Mkazi Mwandamizi Monika Ndyekobora aliyepata udhuru.

Alisema upande wa mashtaka umeshindwa kufika mwisho katika kukamilisha upelelezi wa kesi hiyo.

Alisema upande wa Jamhuri kila mara wamekuwa ukitoa ahadi zisizotimia kuhusu shauri hilo na kutoa onyo chini ya mahakama hiyo kuwa ifikapo Januari 27 mwaka huu, wanatakiwa kuja na taarifa thabiti kuhusu upelelezi na uhitimishaji wanaouahidi mara kwa mara mahakamani.

Onyo hilo lilikuja muda mfupi baada ya mwendesha mashtaka, Mwanahawa Changale kudai mahakamani kuwa ukamilishaji wa kupitia jalada hilo na uamuzi wake haujakamilika huku akiomba kupangiwa tarehe nyingine.

Aliiarifu mahakama hiyo kuwa mapitio ya jalada la kesi hiyo hayajakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa na pengine siku hiyo wawasilishe taarifa kamili.

Hata hivyo, kauli hiyo ilipingwa na wakili wa utetezi, Erick Mutta ambaye alisema kuwa Januari 5 mwaka huu upande wa Jamhuri ukiwakilishwa na Mwanahawa Changale, ulidai mahakamani kuwa Januari 13 (jana) ungekuja na majibu ya msingi kuhusu kitakachoendelea kwenye kesi hiyo.

Wakili Mutta aliiomba mahakama itumie mamlaka yake kuihoji Jamhuri kuhusu uthabiti wa kauli zake kwa kuwa mara kadhaa upande huo umekuwa na taarifa zinazobadilika mara kwa mara, jambo ambalo linamnyima haki mteja wake.

Alitaja kuwa mteja wake sasa ana zaidi ya miezi 10 mahabusu na kama jalada linapanda kwa jaji au vinginevyo ifahamike kwa kuwa haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa.

Katika hatua nyingine, kesi namba 10/2022 inayomkabili Mfalme Zumaridi na wenzake wanane iliyotarajiwa kutolewa hukumu jana, haikutolewa hukumu kufuatia Hakimu Monika Ndyekobora anayesikiliza kesi hiyo kupata udhuru.

Akiahirisha kesi hiyo, Hakimu Sumari alisema Hakimu Ndyekobora amefiwa na ndugu yake na hivyo kushindwa kufika mahakamani na kuelekeza kuwa kesi hiyo itatolewa hukumu Januari 25 mwaka huu



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# ACT yaibwaga CUF kortini

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Zanzibar imetupilia mbali maombi ya Chama cha Wananchi (CUF) ya kutaka Chama cha ACT Wazalendo kiamuliwe kulipa fidia ya Sh. milioni 600 kwa kuharibu samani za ofisi, bendera na kadi za uanachama kwenye ofisi za chama hicho Zanzibar na Pemba.

Hukumu hiyo ya mahakama ilitolewa juzi mbele ya Jaji George Kazi baada ya kupitia malalamiko ya Bodi ya Wadhamini ya CUF dhidi ya ACT Wazalendo, Zitto Kabwe na wenzao 18.

Wakili wa CUF, Mashaka Ngole katika madai aliyowasilisha mahakamani, alidai walalamikiwa walipaka rangi yao kwenye ofisi za CUF Zanzibar na Pemba, waliharibu kadi za uanachama, waliharibu samani za ofisini, walishusha bendera ya CUF na kupandisha bendera ya ACT Wazalendo.

Walalamikaji waliiomba mahakama itoe amri dhidi ya walalamikiwa na wakala wao ya kurejesha hadhi ya ofisi za CUF.

Pia waliomba mahakama iwaamuru walalamikiwa kulipa gharama za samani, bendera, kadi walizoharibu na fidia ya kupaka rangi ya ACT Wazalendo kwenye ofisi za CUF.

Walalamikaji hao waliomba kulipwa fidia ya Sh. milioni 500 na Sh. milioni 100 kwa hasara waliyopata ambapo jumla waliomba walipwe Sh. milioni 600.

Pia waliomba mahakama iwaamuru walalamikiwa kulipa gharama za kesi.

Walalamikaji walikuwa na mashahidi wanne, sehemu ya ushahidi wao ni madai ya kwamba Machi 18 mwaka 2019 walalamikiwa wa pili Salim Bimani, Joram Bashange, Ismail Jussa, Nassoro Mazrui, Thubeit Khamis Faki, Saleh Nassoro Juma, Awadh Ali Said, Ali Abdallah na Zahra Ali Hamad walihamia ACT Wazalendo.

Walalamikiwa hao wanadaiwa kushiriki oparesheni ya 'shusha Tanga, pandisha Tanga' na kinyume cha sheria walibadilisha rangi ya bendera, wakaweka bendera za ACT Wazalendo, waliharibu kadi za uanachama na samani za ofisi za CUF.

Katika utetezi, walalamikiwa wakiwakilishwa na Is - haq Shariff walidai wakalamikaji si wamiliki wa mali hizo zinazolalamikiwa na kwamba hakuna sehemu yoyote kwenye kitabu palipoandikwa kuwa ni wamiliki hivyo wakaomba maombi yatupwe.

Katika hukumu ya mahakama, Jaji Kazi alisema ushahidi wa walalamikaji hautoshi kuthibitisha kuwa ni wamiliki halali wa mali zinazobishaniwa.

"Ili kuonyesha unamiliki halali nyumba au jengo unatakiwa kutoa mahakamani ushahidi wa umiliki, mfano hati, lakini walalamikaji walishindwa kuwasilisha ushahidi huo.

"Kutokana na ushahidi uliotolewa, mahakama inaona walalamikaji wameshindwa kuthibitisha umiliki wao, maombi yaliyowasilishwa hayana msingi yanatupiliwa mbali kwa gharama," alisema Jaji Kazi.

## Mbaroni tuhuma za kumnajisi mwanawe

**Na Neema Hussein,** MPANDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi linamshikilia Augustino Michese (44) kwa tuhuma za kumnajisi mtoto wake mwenye umri wa miaka 16 huku akimtishia kumchoma kisu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame alisema tukio hilo lilitokea kijijini Isinde wilayani hapa.

Alisema mtuhumiwa alikuwa akitoka chumbani kwake na kumwingilia binti yake mara kwa mara nyakati za usiku, binti huyo alikuwa analala sebuleni.

Kamanda alisema mtuhumiwa alimtishia mtoto huyo kuwa akipiga kelele au kusema sehemu yoyote, atamchoma kisu.

Alisema kuwa mama mzazi wa binti huyo ana matatizo ya ugonjwa wa akili, hivyo mtuhumiwa alitumia nafasi hiyo kumfanyia ukatili huo mtoto wake.

Mbali na hilo, jeshi hilo pia linawashikilia watu sita kwa tuhuma za kudaiwa kuua mtu ambaye hajatambulika jina wala sura huku chanzo kikidaiwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Kamanda Makame alisema tukio hilo lilitokea Kata ya Ugala wilayani Mpanda na kwamba polisi walipokea taarifa za mwili huo kuelea ndani ya maji ya Mto Ugala, mtu huyo akikadiriwa kuwa na umri wa kuanzia miaka 40.

Alisema kuwa baada ya mwili huo kuopolewa, ulifanyiwa uchunguzi wa kitabibu na kubainika mwili huo kuwa na majeraha sehemu ya kulia na kushoto katika kichwa chake.Kamanda Makame alisema kuwa baada ya msako kufanyika, walikamatwa Sudi Athuman (44), Sangalo Said (25), Mrisho Hamis (29), Juma Kanyama (53), Malima Antony (35) na Tausi Hamis (38), wote wakazi wa Ugala.

Alisema katika uchunguzi wa awali unaonyesha marehemu alifumaniwa na mke wa mtu ndipo watuhumiwa walimshambulia kwa kumpiga kisha kumtupa mtoni.

"Hata hivyo, watuhumiwa wa matukio yote wanaendelea kuhojiwa na mara baada ya upelelezi kukamilika, watafikishwa mahakamani," alisema.

# Wafanyabiashara walia na miundombinu sokoni

**Na Christina Mwakangale**

WAFANYABIASHARA wa masoko ya Kigogo, Magomeni na Makumbusho katika Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam wameiomba serikali kuwatatulia kero zinazowakabili, ikiwamo uchakavu wa miundombinu ya majitaka, umeme na huduma zingine muhimu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana baada ya Mwenyekiti wa Chama Cha Wafanyabiashara Wilaya ya Kinondoni, Abdalah Mwakilima kutembelea masoko hayo na kuzungumza na wafanyabiashara hao, walibainisha kero hizo zinazokwamisha kufanya biashara vizuri kutokana na kukosekana miundombinu rafiki.

Mussa Kunambi, mchuuzi wa nyanya na mboga, aliiomba waruhusiwe kufanya biashara kwenye maeneo ya chini kutokana na kukosa wateja kwa kuwa kufanyia biashara gorofani kunawaletea hasara na bidhaa zao kuoza.

Mfanyabiashara wa nguo za mtumba, Abass Ramadhani alilalamika wanafanya biashara kwenye mazingira hatarishi kwa kuwa chemba za maji machafu ziko wazi, hivyo maji yanayotoa harufu na baadhi ya chemba zinatoa uchafu kutoka juu ya gorofa.

"Tunakumbana na wizi wa mali, hasa nyakati za usiku kwani tangu tupangiwe eneo hili ni takribani miezi mitatu. Kiukweli kufanya biashara ya mitumba kwenye mazingira magumu ya kukosekana kwa umeme ni shida.

"TANESCO wamewahi kuja hapa na kupima lakini hakuna majibu mpaka sasa hatujaletewa umeme, hatuna amani na mali zetu zinaibwa," alisema Ramadhani.

Baadhi ya wafanyabiashara wa Soko la Makumbusho walidai uongozi wa soko uliopo unawaendesha kwa mabavu na vitisho huku wengine wakiambiwa vizimba vya biashara zao vinazuia magari kuingia na kutoka.

Mwakilima aliwahakikishia wafanyabiashara hao na wateja waliokutwa huko kuwa kero zote zinazowakumba atazifikisha sehemu husika, ili kupatiwa ufumbuzi huku akiwataka kuendelea kuchapa kazi kwa bidii.

Alisema ataendelea kufika kwenye masoko hayo mara kwa mara ili kuhakikisha kero zinazowakumba wafanyabiashara hao zinaondolewa na kuwawezesha kufanya biashara zao katika mazingira safi na salama.

"Ndugu zangu, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Godwin Gondwe pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri yetu wanafahamu kwamba tuna kikao hapa, hivyo ninaomba mnieleze kero zinazowakumba, ili niwapelekee na kuzitafutia ufumbuzi, ninawaomba sana tushirikiane na viongozi wetu," alisema Mwakilima.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2019/20, mbali na mambo mengine, inabainisha hali mbaya ya masoko kwenye miji mbalimbali nchini.

Katia hoja yake, CAG Charles Kichere anapendekeza halmashauri zitimize wajibu wake wa kurejesha sehemu ya mapato yatokanayo masoko ili kuboresha miundombinu ya masoko hayo. Utaratibu huo upo kisheria.

Mwaka 2018, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu hali ya masoko ya bidhaa za vyakula mkoani Dar es Salaam, ikibainika halmashauri zinakusanya mapato kutoka kwenye masoko hayo pasi na kuboresha miundombinu yake, hali inayoakisi dhana ya ng'ombe anayekamuliwa bila kupewa malisho.

# Mkurugenzi matatani madai ya kuuza viwanja 2 kwa bil. 1/-

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima amefikisha ombi kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI la kutenguliwa uteuzi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Sekiete Yahya kwa madai ya kukiuka maelekezo ya Kamati ya Usalama Wilaya ya Septemba 28 mwaka jana kuhusu uuzwaji wa viwanja.

Kamati hiyo ilizuia uuzwaji wa viwanja Na. 194 na 195 vilivyopo kwenye Mtaa wa Rwegasore katikati ya jiji hilo, lakini wao waliamua kuviuza kwa Sh. milioni 500 kila kimoja.

Malima amesema kuwa ofisi yake imeandika barua hiyo kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kutokana na mkurugenzi huyo kuonyesha alichokiita utovu wa nidhamu mara kwa mara kwa viongozi wenzake na kuomba hatua zichukuliwe kwa madai kuwa hafai kuendelea kuwa katika mkoa huo.

"Tumemkuta Mkurugenzi wa Jiji na makosa makubwa ya kukiuka maelekezo ya Kamati ya Usalama Wilaya na ameonyesha kutokuheshimu mamlaka zilizo juu yake kwa utovu huo wa nidhamu alioufanya ambapo alitengeneza hoja ya kuuza viwanja hivyo isivyo halali na tumebaini kuwa endapo vingeuzwa kwa njia ya mnada vingeuzwa kwa zaidi ya Sh. milioni 500 kila kimoja," alisema Malima alipozungumza na waandishi wa habari jana.

Alikumbusha kuwa Septemba 28 mwaka jana, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya iliitaka Halmashauri ya Jiji isiviuze viwanja hivyo bila ya idhini ya kamati hiyo lakini wao wakaamua kuviuza kwa Sh. bilioni moja kwa kisingizio kuwa wamepata rukhsa ya kuuza viwanja hivyo kutoka Ikulu," Malima alisema.

Katika hatua nyingine, Malima alitangaza kuwasimamisha kazi kwa siku saba kupisha uchunguzi watumishi wanne wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza huku akitoa ombi kwa Ofisi ya Rais Samia Suluhu Hassan kutengua uteuzi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo kutokana na madai ya utovu wa nidhamu.

Waliosimamishwa kazi kuanzia jana ni pamoja na Mkuu wa Idara ya Ardhi, Robert Phales, Ayubu Kasuka Halima Nassor na Yuster Zephrine.

Alisema ofisi yake imeunda kamati ya kuchunguza sakata hilo kwa siku saba itakayoongozwa na Mkurugenzi wa Maadili wa Kanda ya Ziwa, Godson Kweka huku ikihusisha wataalamu kutoka Ofisi za TAKUKURU, Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Alifafanua kuwa awali Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilifanya uchunguzi na kubaini kuwa viwanja hivyo vimeuzwa kinyemela bila kumtaarifu Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana na halmashauri imekiri kuviuza na kusema wamefanya hivyo kwa rukhsa ya Ofisi ya Rais Ikulu, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi jambo ambalo si kweli.

"Viwanja hivi haviruhusiwi kuuzwa, kufanyiwa ujenzi wala kuendelezwa kwa namna yoyote mpaka pale suala hili litapomalizika na endapo itaonekana wamiliki wanastahili kuendelea, watapata taarifa na kwa upande wa halmashauri ninaagiza fedha zilizopatikana kwenye uuzwaji wa viwanja hivyo zisitumike ili itapobainika kumekuwa na ukiukwaji wa uuzwaji, basi wamiliki watarejeshewa fedha zao," Malima alisema.

Vilevile, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilitoa Onyo kali kwa Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, watumishi wa Idara ya Fedha na Uhasibu, Ofisa Ununuzi, Mwanasheria na Mkaguzi wa Ndani ikiwataka kujitathmini kwenye utendaji wao kwa kuwa wameonekana kutosaidia halmashauri ipasavyo na itatoa onyo kali kupitia Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa.

"Mwanza haiwezi kuwa kichwa cha mwendawazimu kwamba kila mmoja anakuja kupiga fedha, kama watu wameingia kufanya tamaa na kuhusika na suala hili, basi kwa dhamira yetu kama viongozi wa mkoa tutakwenda kutoa mfano kwenye suala hili kwa kutoa adhabu kali," alionya Malima.




Lundo la takataka likiwa limetelekezwa bila kuzolewa katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachohatarisha usalama wa afya za wateja na wafanyabiashara sokoni hapo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waandishi wa habari kunolewa umuhimu wa kutunza ushoroba

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** BAGAMOYO

CHAMA cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) kupitia ufadhili wa Shirika la Msaada la Marekani (USAID), kimetoa mafunzo kwa waandishi wa habari 25 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu uandishi wa habari za uhifadhi maliasili na mazingira.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani juzi, Mkurugenzi wa JET, John Chikomo alisema mafunzo hayo ni mwendelezo wa mafunzo ya uhifadhi maliasili na mazingira awamu ya pili baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza na kupata mafanikio.

Alisema awali walitarajia waandishi wa habari waliopatiwa mafunzo hayo kuandika habari 150 zenye tija kuhusu uhifadhi wa wanyamapori na mazingira, wakivuka lengo na kuandika habari 254.

Mkurugenzi huyo alisema mafunzo ya awamu hii yamejikita kwenye utunzaji wa shoroba za wanayamapori ili jamii ipate kuelimishwa namna ya kutunza na kuhifadhi kwa kuwa nyingi zimetoweka kutokana na shughuli za binadamu ikiwamo kilimo.

"Uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na wanyamapori na unaleta faida kwa wanyamapori na binadamu ikiwamo maendeleo ya shughuli za kiuchumi kama vile watalii," alisema Chikomo.

Mwenyekiti wa JET, Dk. Ellen Otaro alivitaka vyombo vya habari kuandika habari za uhifadhi na utunzaji wa mazingira na kulipa umuhimu suala la ushoroba ili kuandika habari nyingi zaidi zenye tija na kuleta mabadiliko katika nchi.

Meneja wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, John Stiven alisema kuwa kupitia mradi huo wa miaka mitano, wamemaua kufanya kazi katika korido saba Tanzania ili kuchochea utunzaji wa viumbe hai ambavyo haviwezi kupatikana sehemu zingine. Alisema maeneo hayo yanapata athari kubwa za uvamizi ikiwamo kubadilishwa matumizi kutoka uhifadhi kwenda kilimo na makazi na serikali imevipa vipaumbele shoroba zenye umuhimu na kufanyiwa kazi.

"Tunakata kuona maeneo hayo yanalindwa na tunapenda kuona shoroba zinaendelea kuwapo hata baada ya mradi na kuwapa fursa za kiuchumi wananchi walio karibu na shoroba hizo ili kuziendeleza," alisema.

Aliongeza kuwa kutokuwapo shoroba kuna athari kubwa kwa kuwa hifadhi na mbuga zinazolindwa zitakuwa kama visiwa na wanyama hawatoweza kutoka hifadhi moja kwenda nyingine, hivyo kuwa na wanyama dhaifu na kupata ugonjwa na hatimaye kutoweka.

Meneja Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi wa Mradi wa USAID Tuhifadhi Mazingira, Dk Elikana Kalumanga alisema kwenye mapitio ya wanyama kuna fursa nyingi za kijamii, kiuchumi na kiikolojia kwa sababu katika hifadhi hizo kuna ufugaji wa nyuki na utalii.

Alisema wananchi walio karibu na maeneo ya hifadhi, hawatoathirika sana na athari za mabadiliko ya tabianchi kulinganishwa na wananchi wanaoishi mbali na maeneo hayo.

## Kesi kuchoma mke magunia ya mkaa yapigwa kalenda

**Na Grace Gurisha**

UPELELEZI wa kesi ya mauaji inayomkabili mfanyabiashara Khamis Luwonga (38) anayetuhumiwa kumuua mkewe Naomi Marijani kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, haujakamilika.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Wakili wa Serikali Adolf Valundami mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

Wakili Valundami alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo wanaiomba mahakama iwapangie tarehe nyingine ya kutajwa.

Baada ya kutolewa kwa taarifa hiyo na ombi hilo, Hakimu Ngimilanga aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 26 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

Awali mshtakiwa Luwonga alidai mke wake Naomi kila siku alikuwa anamwomba Mungu afe kuliko kuendelea kuishi katika ndoa yao na alikuwa anang'ang'ania kifo chake kwa nguvu na kwamba sasa mtoto wao anaishi bila wazazi. Pia alidai kifo cha Naomi hakikusababishwa na yeye peke yake, bali kuna wengine waliyohusika zikiwamo familia za pande zote za mbili, maofisa wa polisi na watumishi wa ngazi za chini za serikali.

"Kama tukio nililoshshtakiwa nalo watanzania wanaangalia uhalibifu uliotokea, hawaangalii chanzo nini, nina maumivu makubwa sana ya kifo cha mke wangu kipenzi Naomi kwa sababu ya baadhi ya watu wanaodharau matukio.

"Walipaswa kuzuia mambo ya hatari kutokea na siyo kusubiri uhalibifu kutokea, Hata vitabu vya dini vinaeleza hayo, kwenye Quran na kwenye Biblia ukisoma utaona ninachokizungumzwa kwamba ukimwona mtu anataka kukengeuka unamweka sawa," alidai Luwonga.

Katika kesi hiyo ya muaaji namba nne ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole wilayani Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

Inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo baada ya kumuua mke wake, alimchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa kisha alichukua majivu ya mwili wa marehemu na kwenda kuyafukia shambani kwake.

## Silinde atoa maagizo kwa wakuu wa mikoa na wilaya

**Na Francis Godwin,** IRINGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, ametoa maagizo manane kwa wakuu wa mikoa na wilaya katika kusimamia watendaji wa elimu kuanzia ngazi za kata hadi mkoa.

Maagizo hayo yanalenga kufanikisha utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari nchini na kusisitiza hadhi za walimu kuheshimiwa.

Silinde aliyasema hayo juzi katika kikao kazi cha uboreshaji wa usimamizi wa elimu ya msingi na sekondari nchini kilichoandaliwa na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na walimu na wadau mbalimbali wa elimu mkoa.

Alisema ili kufikia malengo ya upatikanaji wa elimu bora, serikali imekuja na mikakati hiyo minane ambayo itasaidia kila mmoja kujua wajibu wake.

Awali, Silinde alisema kwa mwaka 2022 pekee, serikali ilitoa Sh. bilioni 62 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 8,000 kwa wanafunzi wa sekondari jambo ambalo limesababisha wanafunzi 1,073,402 ambao walifaulu mtihani wa darasa la saba kupata madarasa ya kusomea.

Alisema katika mpango wa sasa, serikali ina mpango wa kujenga shule za bweni za kisasa kwa ajili ya wasichana kila mkoa nchi nzima.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, alisema mkoa huo unakabiliwa na upungufu wa walimu wa shule ya msingi 1,100 na wa sekondari ni walimu 913 jambo ambalo linasababisha changamoto katika utoaji wa elimu sahihi kwa wanafunzi.

Dendego pia alisema kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 1,800 kwa shule za msingi na sekondari.

Katika hatua nyingine, Dendego alisema hadi kufikia Januari 6, mwaka huu, mkoa umefikia asilimia 72 ya uandikishaji wa wanafunzi wa awali na asilimia 78 kwa wanafunzi wa darasa la kwanza.

# Ununuzi vipande waingiza bil. 12.95/- miezi miwili

**Na Beatrice Moses**

MATUMIZI ya teknolojia ya kisasa inayotumika kwenye mauzo ya vipande vya Faida Fund imerahisisha uwekezaji wa pamoja kwa watu 3,800 kuwekeza jumla Sh. bilioni 12.95 ndani ya miezi miwili.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investment (WHI), Dk. Fred Msemwa, alisema teknolojia hiyo imesaidia ununuzi kufanywa kwa urahisi na kufikia asilimia 173 kiwango ambacho ni kikubwa tofauti na makisio waliyoweka.

"Hatua hii imeonyesha kuwa watu wameuamini mfuko wa Faida Fund kuwa njia rahisi ya kununua vipande. Kuna mfumo maalum wa kiteknolojia umeongeza kasi ya ununuzi wa vipande. Bila kulazimika kufika katika ofisi za Faida Fund, mwekezaji au wawekezaji wananunua kupitia simu," alisema.

Dk. Msemwa alisema wawekezaji hao wa kipato cha chini na kati, wakiwamo wavuvi, wakulima, waendesha bodaboda, mamalishe, baadhi ya taasisi binafsi na za serikali, ambao ndio waanzilishi wa mfuko huo, watahakikisha wanasimamia ipasavyo ili malengo yaliyowekwa yatimie.

"Mauzo ya awali ya vipande katika mfuko wa Faida yalifunguliwa Novemba, 2022 na kufungwa Desemba 31, 2022 na Sh. bilioni 12. 95 zimepatikana ikilinganishwa na Sh. bilioni 7.5 zilizotarajiwa kupatikana awali," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Msemwa, bei ya kipande ni Sh. 100 na kiwango cha chini cha uwekezaji ni Sh. 5,000 na 10,000 na hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza. Fedha hizo za uwekezaji zitawekezwa katika masoko ya hatifungani asilimia 60 na masoko ya fedha asilimia 40.

Mkuu wa Idara ya Mitaji na Masoko wa benki ya CRDB, Masumai Ahmed, alisema Faida Fund ni miongoni mwa mifuko saba ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na benki hiyo.

Ahmed aliwahakikishia wananchi kuwa Faida Fund ni mahali salama pa kuwekeza na kwamba CRDB ina uzoefu wa kutosha katika kusimamia usalama wa fedha zinazowekezwa, hivyo ni wazi kuwa wanaowekeza watanufaika na malengo yaliyowekwa.

"CRDB ina zaidi ya mawakala 25,000 nchini, hivyo wanaowekeza kwenye mfuko huo wanatumia mawakala katika kufanikisha kununua vipande," alisema.



Mafundi wakiweka makaravati kwa ajili ya mifumo ya maji ya mvua kwenye ujenzi unaoendelea wa miundombinu ya mabasi ya mwendo kasi, katika Barabara ya Kawawa, eneo la Kigogo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wananchi 24,000 kunufaika mradi wa maji

**Na Joseph Mwendapole**

UTEKELEZAJI wa mradi wa maji Majohe katika wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, unatarajiwa kuwanufaisha wananchi 24, 000 utakapokamilika.

Mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), umeendelea kutekelezwa kwa kasi na unatarajiwa kukamilika Juni, mwaka huu.

Akizungumzia hatua mbalimbali za mradi ulipofikia, Msimamizi wa Miradi Mkoa wa Kihuduma wa DAWASA Ukonga, Mhandisi Ibrahim Kazumba, alisema utekelezaji wa mradi unaendelea vizuri ambapo mpaka sasa jumla ya kilomita 16 za mabomba makubwa ya kusafirisha majisafi zimeshalazwa na kufukiwa.

Aliongeza kuwa kwa wiki hii, kazi ya uchimbaji na ulazaji wa mabomba ya inchi mbili na tatu imefanyika kwa umbali wa kilomita mbili.

"Utekelezaji wa mradi huu unaenda vizuri, tumefanikiwa kujenga mtandao wa mabomba wa kilomita 16 mpaka sasa na kazi inaendelea ili kukamilisha eneo lililobaki," alisema Kazumba. Aliongeza pia kuwa huo ni mradi wa kipaumbele ambao unatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za mamlaka kwa gharama ya Sh. bilioni 4.2 kwa lengo la kuondoa changamoto ya maji kwenye eneo hili la Majohe.

Kazumba alibainisha kuwa mradi huu ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/23 na unaenda kunufaisha wakazi takribani 24,000 wa eneo lote la Majohe.

"Kupitia kazi hii maeneo ya kwa Ngozoma, Kwaharisi, Majohe B, Majohe Songas, kwa Diwani na Bombambili, itapata huduma," alisema. Pia alitaja mitaa itakayonufaika na mradi huo kuwa ni pamoja na Majohe Kichangani, Majohe Rada, kwa diwani, Viwege, Bombambili na Kivule.

"Tunatarajia kukamilisha utekelezaji wa mradi huu mwezi wa sita mwaka huu ambapo wakazi wengi wataanza kupata huduma ya majisafi," alisema Mhandisi Kazumba.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Majohe, Ramadhan Mayala, alisema mradi huo ni muhimu sana kwa kuzingatia shida ya maji iliyopo kwenye Kata hiyo wakazi wengi wanahitaji majisafi kwa kuwa kwa sasa wanatumia maji ya visima. Alisema jitihada hizo ni za kupongezwa kwa kuwa zitasaidia kuondoa malalamiko ya wananchi kwa Serikali yao.

Kwa upande wake, mkazi wa Majohe, Zuhura Shabani, alisema huduma ya majisafi kwao imekuwa ni ndoto ya miaka mingi kwa kuwa hawajawahi kupata kabisa huduma.

"Tunashukuru kwa jitihada hizi za DAWASA zinazofanyika za kuleta huduma kwenye eneo hili maana ndio matarajio tuliyonayo wananchi wengi wa huku," alieleza.

Nae Paschal Richard, mkazi wa Mtaa wa Majohe Kichangani, alisema mradi huo utakuwa suluhisho la kudumu la shida ya maji kwenye eneo hilo.

"Ni hatua nzuri ambayo DAWASA imeifanya ya kutekeleza mradi huu maana ukikamilika utakuwa msaada mkubwa kwa wananchi wengi," alisema Richard.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu, wachezaji epukeni kukomoana dirisha dogo

**DIRISHA** dogo la usajili wa wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League, Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania linatarajiwa kufungwa rasmi ifikapo kesho saa 5:59 usiku.

Kalenda hiyo ilitangazwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na kwa dunia ya sasa dirisha likishafungwa, hakuna nafasi ya kuomba kufanya usajili au kuhamisha mchezaji nje ya muda huo.

Lengo la dirisha hilo kufunguliwa ni kutoa nafasi kwa timu kuboresha vikosi vyao katika idara ambazo wamebaini zina mapungufu ili kujiimarisha na kuifanya timu husika kurejea kwenye ushindani.

Lakini pia hutumika kwa wachezaji kuomba kuondoka au kuvunja mkataba na timu yake ya sasa na kujiandaa kwenda kutafuta changamoto mpya baada ya kukosa nafasi ya kucheza na uamuzi huo hufanywa kwa ajili ya kuhitaji kulinda kiwango cha mchezaji.

Wapo ambao tumeshuhudia wanapelekwa kwa mkopo katika timu nyingine na kufanikiwa kuonyesha ubora na hatimaye kurejea kwa heshima kule walikoondoka lakini pia kwenda kuzisaidia timu zilizohitaji mchango wao kutokana na ubora wanaoufahamu.

Tunafahamu pia wapo wachezaji wanaotaka kutumia kipindi hiki kwenda kupata maslahi bora zaidi ukilinganisha na kile alichokuwa analipwa katika timu yake ya sasa, baada ya kubaini thamani yake imeongezeka na anastahili kupata mshahara mnono pamoja na kiasi kikubwa cha ada ya usajili.

Katika dunia ya sasa ambayo inaongozwa na sheria, kanuni na taratibu, ni vyema kila upande ukaheshimu mikataba ambayo walisaini huko nyuma na kukubaliana na hali halisi iliyopo kwa sasa.

Kama tumeshuhudia klabu mbalimbali zikivunja mikataba na makocha au wachezaji wake, vile vile tuwe wepesi wa kuheshimu na kukubali inapotokea mchezaji au mwajiriwa mwingine wa klabu anapofanya uamuzi wa kuachana na timu moja na kuelekea kwingine.

Mwaka jana tulishuhudia aliyekuwa Msemaji wa Simba, Haji Manara, alitangaza kuachana na klabu yake ya tangu utotoni na kujiunga na watani zao wa jadi, Yanga, lakini kutokana na taaluma yake, aliondoka huku akitoa lawama kwa baadhi ya mabosi wake, jambo ambalo hatutegemei kulioka kwa wachezaji au makocha wanaohitaji kukutana na changamoto mpya.

Haikupita muda mrefu, tulishuhudia tena aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi, Senzo Mbatha, raia wa Afrika Kusini, ambaye alieleza anaachana na Simba na kurejea kwao kuungana na familia yake, kufanya kazi Tanzania kuliipa changamoto familia yake na hivyo akaamua kubwaga manyanga.

Naye haikupita muda mrefu, akatua Yanga na kusema yeye anafanya kazi yake kwa weledi, hana mapenzi na Simba, anaomba aheshimiwe kwa uamuzi huo, na aliahidi angeisaidia klabu hiyo ya Mtaa wa Twiga na Jangwani kufanya vyema kwenye Ligi Kuu Tanzania, Bara, Kombe la FA, jambo ambalo alimudu.

Kama watendaji hao wamehama kutoka klabu moja na kwenda nyingine, tena timu ambazo zina ushindani mkubwa, umefika wakati mabosi wakawakubalia wachezaji wao ambao wanahitaji kuvunja mikataba au wanaoomba baraka ya kwenda sehemu nyingine kutafuta maisha.


Huko nyuma ilionekana ni jambo lisilowezekana kwa mchezaji kuilipa klabu fedha ili kuvunja mkataba maana tulizoea kuona timu zikifunguliwa mashtaka kwa kuvunja mikataba kinyume na sheria na baadaye kutakiwa kulipa fidia ya uamuzi uliofanyika, sasa tunashuhudia kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' ameshikilia msimamo wake wa kuachana na Yanga na anahitaji kwenda kusaka changamoto mpya.

Shauri hili na mengine ambayo yamefikishwa katika Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF yanatakiwa yatolewe uamuzi kwa kuzingatia vipengele husika vilivyoko kwenye mikataba yao na si vinginevyo.

Kuheshimu vipengele vya mikataba itasaidia kufanya uamuzi wa haki na si kutumia busara au nguvu za 'nje' ambazo huko mbele huvuruga weledi wa taasisi hiyo yenye mamlaka ya kusimamia soka hapa nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Sakata la kiungo Fei Toto, SPUTANZA mbona kimya?

**NI** wiki tatu au zaidi kuna sakata ambalo linaendelea kuhusu Feisal Salum 'Fei Toto' dhidi ya klabu yake ya Yanga.

Ni mgogoro wa kimkataba baina ya pande hizo mbili. Kiungo huyo amevunja mkataba lakini klabu hiyo haitaki kukubaliana na uamuzi wa mchezaji huyo kutoka Zanzibar.

Fei Toto anataka kuondoka, lakini klabu yake inamwambia kama anataka kuondoka basi afuate taratibu zinazotakiwa. Kuna mengi yameelezwa na kutokea, ikiwamo Yanga kufungua shauri katika Kamati ya Sheria na Hadhi ya Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na huko wakaamua kuwa Fei Toto ni mchezaji halali wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara.

Nimeona mawakili wa mchezaji huyo wakiwa hawajaridhika na uamuzi huo, na kwa sasa wanajiandaa kwenda katika Mahakama ya Usuluhishi wa Masuala ya Michezo (CAS). Nadhani wao wanaamini haki haijatendeka kwa mteja wao.

Kwa sababu haya ni masuala ya mikataba na kisheria, basi tunawaachia wanasheria ambao waliotoa uamuzi na hao wanaotaka kwenye CAS.

Ila nilichoshangaa katika suala hili la Fei Toto ni ukimya wa Chama cha Wachezaji Soka Tanzania (SPUTANZA).

Chama hiki kiko kwa ajili ya wanasoka Tanzania nzima, lakini kwenye shauri hili naona wako kimya kiasi mchezaji anaonekana kama yupo peke yake sana.

Sisemi kama SPUTANZA wao wangeamua chochote, lakini hata wao kuna kitu wangesema kuonyesha wameguswa na hilo kama wengine walivyokuwa wakilisemea. Tumeona huko nyuma chama hicho kikitoa matamko, kusimama na wachezaji, angalizo na hata kuwaonya wachezaji kuhusu masuala mbalimbali yanayofanana na haya, lakini hili imekuwa kinyume chake.

Mwaka 2015, SPUTANZA ilivalia njuga suala la Juma Kaseja na Yanga, ambapo iliiandikia barua TFF imtangaze mlinda mlango huyo ni mchezaji huru.

Hiyo ni baada ya Yanga kumfungulia mashtaka mchezaji huyo katika Mahakama ya Kazi ikimtaka Kaseja kuwalipa fedha wakimtuhumu kuvunja mkataba na timu hiyo.

Na kweli baadaye sakata liliisha na Kaseja akawa mchezaji huru.

Mwaka huo huo kulikuwa na kesi ya Ramadhani Singano 'Messi' wakati huo akiitwa dhidi ya Simba. Nayo ilikuwa ni ya kimkataba.

SPUTANZA iliwasilisha TFF nyaraka muhimu kuhusu mkataba wa winga huyo na Simba ili kumaliza mvutano uliojitokeza.

Kulikuwa na mvutano kati ya Messi na uongozi wa Simba baada ya winga huyo kudai kutoutambua mkataba wa miaka mitatu kati yake na klabu hiyo ya Msimbazi uliopo TFF.

Iliwasilisha nyaraka za mikataba miwili ya Messi na Simba baada ya kubaini kuna utata katika mkataba ambao mchezaji huyo akadai kutoutambua, huku yeye akiutambua ule ya miaka miwili.

Mwaka 2016, SPUTANZA iliingilia kesi ya klabu ya Simba kumfungia mchezaji wake Hassan Kessy kwa mechi tano baada ya kumchezea rafu mbaya mchezaji wa Toto African wakati huo, Edward Christopher.

Hata hivyo meneja wake, Athumani Tippo, alipinga hilo na kupeleka malalamiko huko.

Hiyo ni mifano michache tu inayoonyesha chama hicho kimefanya kazi kubwa sana kusaidia wachezaji Tanzania na soka kwa ujumla. Kwa hili mbona iko kimya? Imepatwa na nini? Au Fei Toto si mwanachama wao? Au hajaenda kupeleka malalamiko yake huko? Hapa inabidi chama hicho kitoe ufafanuzi hakiwezi kusema lolote, au kufanya chochote mpaka wapelekewe malalamiko rasmi?

Mashabiki wengi wamekuwa wakijiuliza imekuwaje? Mbona hakisikiki kwenye hili? Hata kisiegemee upande wowote ule, lakini kitoe japo msimamo wake na ushauri pia.

## Mkurugenzi JATU kuanza kujitetea

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya JATU Public Ltd, Peter Gasaya (32), anayetuhumiwa kujipatia Sh. bilioni 5.1 kwa njia ya udanganyifu anatarajiwa kuwasilisha hoja zinazohusiana na dhamana yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Januari 2 mwaka huu, Gasaya alisomewa masharti ya dhamana, alitakiwa awasilishe mahakamani Sh. bilioni 2.6 au hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo na pia awe na wadhamini wawili, lakini alirudishwa rumande kwa kushindwa kutimiza masharti hayo.

Taarifa hiyo ya Gasaya iliwasilishwa jana kupitia Wakili wake, Kung'he Wabeya mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Francis Mhina wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa na Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru.

"Mheshimiwa tunaomba tupangiwe tarehe ya karibu kwa sababu kuna hoja tunataka kuziwasilisha kwa hakimu husika, Mary Mrio kuhusiana na dhamana ya mshitakiwa," alidai Kung'he.

Hakimu Mhina alikubaliana na ombi hilo na kupanga tarehe ya karibu ambayo ni Januari 13, 2023, ili upande wa utetezi waweze kuwasilisha hoja zao.

Awali, Hakimu Mrio alimueleza mshitakiwa kuwa pia

ili atatakiwa awe na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho na vitambulisho ambavyo kila mmoja atasaini bondi ya kiasi hicho cha fedha.

Inadaiwa kuwa kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba 31, 2022 mshitakiwa akiwa ndani ya jiji na Mkoa wa Dar es Salaam kama Mkurugenzi wa kampuni hiyo alijipatia Sh 5,139,865,733 kwa njia ya udanganyifu kutoka JATU SACCOS.

Mshitakiwa alichukua fedha hizo kwa madai kuwa atazipanda fedha hizo na kuzalisha faida huku akijua si kweli. Baada ya mshitakiwa kusomewa shitaka lake, alikana kuhusika na tuhuma hizo.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan 'Zungu' (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Diwani wa Kata ya Minazi Mirefu, Godlisten Malisa (kushoto), wakati alipokagua majengo ya SUDECO yanayomilikiwa na Wizara ya Kilimo, jijini Dar es Salaam jana. Diwani Malisa, aliomba wapewe majengo hayo ili wayatumie kwa ajili ya kutoa huduma za kijamii katika Kata hiyo. Wa (pili kulia) ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilala, Said Side. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waathirika tope mgodi wa almasi kuanza kulipwa fidia

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKAZI wa vijiji vya Ng'wanholo na Nyenze Kata ya Mwadau Luhumbo, wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, wataanza kulipwa fidia baada ya kukamilika kwa uthamini wa mali zao kwa kujaza fomu kuonyesha mali zitakazolipwa.

Ofisa Uhusiano wa Mgodi wa Almasi wa Mwadui, Bernard Mihayo, alisema utaratibu wa uthamini umekamilika kwa kujazwa fomu kuonyesha mali watakazolipwa fidia

Wakazi hao ni waathirika wa tope la bwawa la mgodi huo la kuhifadhi maji machafu, baada ya Novemba 7, mwaka jana kingo zake kubomoka na kusababisha tope zito kuvamia makazi ya watu wanaoishi jirani na mgodi na kufunika baadhi ya vyumba, visima vya maji na mashamba.

Baada ya tukio hilo, uongozi wa mgodi ulichukua hatua ya kuwalipia kodi za nyumba walizopanga waathirika hao ikiwa ni pamoja na kupewa huduma zote za kijamii ikiwamo chakula, maji na malazi wakati wakisubiri kulipwa fidia.

Wakizungumza juzi katika kikao cha uthamini wa mwisho wa mali zilizoathiriwa na tope kwa kujaza fomu namba tatu ambayo inaonyesha mali watakazolipwa, waliuomba mgodi huo kuharakisha ulipaji fidia ili kila mtu achukue chake na kutafuta mahali pa kuishi sehemu anayoitaka na sio kupangiwa.

Waathirika hao walisema hata katika vijiji vyao kuna maeneo ya kuishi kwa kuwa sio eneo lote lililoathiriwa na tope na kwamba kuendelea kuishi katika nyumba za kupanga zinazolipiwa na mgodi huo bila kuendelea na shughuli zao za kila siku, inarudisha nyuma malengo na mipango yao.

Rashidi Athumani, mmoja wa waathirika hao alisema maisha yao kwa sasa yamebadilika kutokana na kuwa tegemezi na kuishi kwenye nyumba za kupanga.

Alisema licha ya kupewa huduma zote za kijamii ikiwamo chakula, maji na malazi, lakini wanataka walipwe stahiki zao mapema ili wajitegemee.

Mihayo alisema, hatua inayofuata ni kwenda kwenye fomu namba nne ambayo itaonyesha kiasi cha fedha atakacholipwa kila mmoja na kisha taratibu za malipo kuanza kupitia akaunti za benki.

"Taratibu za uthamini zimefikia ukigoni na wale wote ambao walilalamika kupunguziwa maeneo yao, malalamiko yao yamefanyiwa kazi na sasa hakuna dukuduku tena kila kitu kipo sawa na tutaanza kuwalipa fidia hivi karibuni," alisema Mihayo.

Aliwasihi wananchi kuwa fedha hizo za fidia wakazitumie vizuri kwa kufanya maendeleo, ili waendelee na maisha yao kama zamani na sio kukimbilia mambo ya anasa na kubaki hawana kitu na kurudi kwenye umaskini.

Naye, Mthamini Kiongozi, Richard Sabini, alisema watu watakaolipwa fidia kwa mujibu wa sheria, ni wamiliki wa nyumba na ardhi na sio wapangaji na watalipwa mali walizopoteza na idadi yao ni 180.

Vilevile, Mhandisi Mkuu wa mgodi, Shagembe Mipawa, alisema mgodi umeshafanya ukarabati wa kingo la bwawa lililobomoka, pamoja na kuweka matuta ili kuzuia tope lisivamie tena makazi ya watu.

# TARURA, TANESCO zaagizwa kutoa huduma

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ameziagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kupeleka huduma za umeme na barabara kwenye minara ya simu inayojengwa ili kurahisisha utoaji wa huduma ya mawasiliano kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizindua mnara wa simu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) katika kijiji cha Misughaa, Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida. Alisema, kukosekana kwa huduma za umeme na barabara kwenye minara ya mawasiliano inayojengwa na serikali, kunakwamisha utekelezaji wa kutoa huduma kwa wananchi.

"Kuna changamoto sana kuendesha minara ya simu kwa kutumia umeme wa sola, wakati jua lisipokuwapo mawasiliano yanakuwa ya shida sana kwa wananchi," alisema.

Alisema TARURA pia itengeneze barabara sehemu ambazo zina minara, ili kurahisisha matengenezo na wataalamu kufika kwa wakati kwenye minara inapotokea changamoto.

Mtendaji Mkuu wa TTCL, Peter Ulanga, alisema mnara huo utasaidi kutoa mawasiliano ya simu kwa wananchi wa vijiji vitatu vilivyopko katika Kata ya Misughaa.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF), Justina Mashiba, alisema mfuko huo utaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha mawasiliano yanawafikia wananchi kwenye maeneo yao kwa ajili ya maendeleo. Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Misughaa, waliishukuru serikali kwa kuwafikishia huduma ya mawasiliano ambayo itaondoa tatizo lililokuwa likiwakabili.

# LG yaja na mikakati kuongeza ubunifu kwa maisha endelevu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya vifaa vya kielektroniki ya LG imetangaza mkakati wa mwaka 2023, wenye lengo la kujenga ubunifu kwa ajili ya maisha bora na kuhakikisha maisha endelevu kwa wote.

Mkurugenzi Mtendaji wa LG, William Cho alitangaza hayo jana wakati wa mkutano mkuu wa LG na vyombo vya habari uliofanyika kwenye maonyesho ya Consumer Electronics (CES) 2023 yanayoendelea jijini Las Vegas, Marekani. Katika taarifa yake kwa umma, alisema mpango unaonyesha upatikanaji madhubiti wa uvumbuzi ambao unalenga mahitaji ya wateja kwa dhumuni la kujenga maisha bora kwa kila mmoja, na kujali mazingira.

Alisema mpango ambao umeambatishwa katika mkakati wa 2023 ESG wenye jina la better Life life, na mpango kazi wake uitwao Better Plan ambao unalenga kujenga upatikanaji, urahisi wa bidhaa na huduma kutumiwa na watu wenye ulemavu na wazee.

Cho alisisitiza utayari wa kampuni wa kuchukua changamoto mpya katika mwaka 2023 na kuendelea bila kujali hali yoyote, akigusia kwamba kampuni ya LG imekuwa inafahamu na kuamini kwa dhati kwamba jibu liko kwa mteja.

Alizungumzia ubunifu mkubwa ujao unaolenga wateja katika bidhaa zake za umeme za majumbani, LG OLED ambayo imebadilisha mwonekano kwa wateja walivyokuwa wanangalia televisheni zao.

Alibainisha kwamba kampuni inafanya kazi na washirika wake kutambulisha aina mbalimbali za huduma kupitia LG TVs, ikiwamo mfumo wa elimu kwa njia ya mtandao MasterClass, programu ya mazoezi MaxPro na huduma za metaverse Sansar ambazo zitapanua uzoefu wa wateja na kuwezesha watumiaji wa TV kupata uzoefu mpya katika uangaliaji.

Wakati ambapo inasherehekea kutimiza miaka 10 tangu kuanzishwa, bidhaa za LG OLED inaendelea kuweka viwango vipya vya ubora katika sekta kwa ubora wa picha na uzoefu wa wateja ambao haujawahi kutokea.

Mkurugenzi huyo alizungumzia kuhusu LG Think UP, aina mpya ya vifaa vya nyumbani vinavyoendelea kubadilika; vinavyotoa fursa ya kipekee vinavyoweza kuboreshwa na kubadilishwa kuendana na mahitaji ya mtumiaji. Orodha ya kipekee ya bidhaa zinajumuisha bidhaa za kimapinduzi kama Jokofu la LG lenye MoodUP™, ambayo inaweza kubadili rangi kuendana na mahitaji ya mtumiaji, anavyojisikia au kuendana na mapambo ya jiko.

Cho alisisitiza utayari wa kampuni ya LG kama shirikja lenye uwajibikaji kwa jamii kuweza kufikia maendeleo endelevu. Alitaja ahadi ya kampuniya kuongeza upatikanaji na urahisi wa kutumia bidhaa na huduma za LG kwa walemavu na wazee.

Ahadi hii kama ambavyo inaongozwa na maoni kutoka kwenye Kikundi cha Ushauri cha Walemavu cha LG ('Disabled Advisory Group') -ambacho kinafanyakazi tangu 2021 ambacho kina wajumbe wenye uwezo tofauti tofauti na wataalamu wa ufikivu - kampuni inaendelea kutambulisha bidhaa zisizo na uzuizi ambazo zinaweza kutumiwa na watu wote kwa urahisi.

Katika kukamilisha jambo hili hivi sasa kampuni ya LG inaendesha mashindano ya Teknolojia ya Habari ulimwenguni (Global IT Challenge) kwa vijana wenye ulemavu (GITC) ambayo tangu mwaka 2011 imewawezesha zaidi ya vijana 4,000 kujenga ujuzi katika teknolojia kuondoa mgawanyo wa kidigitali kwa watu wenye ulemavu.

Katika hali hiyo hiyo, wataalamu wa LG wanalenga kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa kwa asilimia 20 katika bidhaa zake 7 kubwa kupitia matumizi yenye ufanisi ya nishati, hata wakati ambapo inalenga kukamilisha mabadiliko yake kuelekea katika nishati mbadala kufikia 2050.



Waziri wa Maji, Juma Aweso (wapili kulia), akikagua ujenzi wajengo la wizara yake, mkoani Dodoma juzi. Kulia kwake ni Msimamizi wa ujenzi huo, Mhandisi Mwajuma Waziri. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mbunge adai madarasa fedha UVIKO-19 kuchakachuliwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE wa Jimbo Songwe, Philipo Mulugo, ameeleza kutoridhishwa na ujenzi wa maabara ya Shule ya Sekondari Gua, uliogharimu Sh. milioni 90 ambao una nyufa.

Alisema mkandarasi ameshalipwa fedha zake zote na kuondoka, jambo ambalo sio sahihi.

Alibaini maabara hiyo kujengwa chini ya kiwango baada ya kufanya ziara juzi ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika jimbo hilo na kukagua shule hiyo mpya yenye miaka minne tangu kuanzishwa.

Alisema mwishoni mwa 2021 serikali ilitoa Sh. milioni 90 za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Ugonjwa wa Virusi vya Corona, UVIKO-19, kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya masomo ya fizikia, kemia na baiolojia.

"Mkandarasi ambaye ni Amani Said Mwizalubi, 'finishing' hajafanya vizuri jengo lina nyufa chini ya sakafu, kwa kweli sijaridhishwa," alibainisha. Mulugo alisema rais anahangaika kutafuta fedha kwa ajili ya maendeleo na yeye mbunge hawezi kukubali kuona fedha zinachezewa na kuahidi kuwasiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ili mkandarasi huyo atafutwe arudie kazi hiyo.

Alisema katika hali ya kushangaza, mkandarasi huyo amepewa zabuni nyingine ya kujenga majengo katika Shule ya Sekondari ya Philipo Mulugo iliyopo kijiji cha Udinde.

Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Songwe, Christian Simba, alisema chama hicho hakikubaliani na ujenzi wa majengo hayo ulivyofanyika na hivyo suala hilo litapelekwa kwenye Kamati ya Siasa ya wilaya lijadiliwe na kutoa uamuzi. Alisema inashangaza kuona jengo hilo la maabara limekamilika kujengwa mwisho wa mwaka jana na kuanza kuweka nyufa.

Alisema serikali inapotoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo lolote inataka kuona linadumu kwa zaidi ya miaka 50 na kuwa mkandarasi aliyepewa zabuni kujenga jengo hilo alitakiwa kuzingatia.

Katibu huyo aliwaagiza viongozi wa CCM wa kata zote wanapoona miradi inayotekelezwa kwenye kata zao watoe taarifa wilayani badala ya kukaa kimya, kwa kuwa pamoja na mambo mengine chama kinapaswa kusimamia miradi ya maendeleo ili ijengwe kwa kiwango kinachokubalika.

# Watiwa mbaroni tuhuma kuiba mbolea ya ruzuku

**Na Thobias Mwanakatwe**

MSAKO unaoendelea kufanywa na Jeshi la Polisi mkoani Songwe, umewanasa watumishi wengine watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani humo, kwa tuhuma za wizi wa mifuko 991 ya mbolea ya ruzuku.

Kukamatwa kwa watumishi hao watatu kunafanya jumla ya watumishi wa halmashauri hiyo waliokamatwa hadi sasa kufikia saba, wakituhumiwa kwa wizi wa jumla ya mifuko 2,917.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Rashid Ngonyani, akizungumza na gazeti hili jana kwa simu aliwataja watumishi waliokamatwa kuwa ni Ofisa Mifugo Kata ya Hasamba wilayani humo, Elizabeth Temba ambaye anadaiwa kujipatia mifuko 311 ya mbolea lakini hana shamba.

Mwingine ni Ofisa Sanifu Mifumo Halmashauri ya Mbozi, Alphonse Nanyanga ambaye alikutwa na mifuko 680 ya mbolea na Mwalimu wa Shule ya Msingi Itete, Mwile Mwashiuya anayedaiwa kuuza mbolea bei ghali ya Sh.85,000 badala ya Sh. 70,000 ambayo ndiyo bei elekezi ya serikali.

Aliongeza kuwa msako zaidi bado unaendelea kukamata wengine na zoezi litakapokamilika jalada litapelekwa katika ofisi ya mashtaka kwa hatua zaidi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Ngonyani juzi alitoa taarifa za kukamatwa watumishi wanne wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi wakituhuma kwa wizi wa mifuko 1,980 ya mbolea ya ruzuku.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Aloyce Madaraka ambaye ni Ofisa mwandamizi Idara ya Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, ambapo alidanganya kuwa ana shamba la ekari 30 na kujipatia mifuko 71 ilhali hana shamba.

Alisema mtuhumiwa huyo pia amewaingizia watu wengine taarifa za uongo na kuchukua mbolea ya ruzuku.

Wengine ni Ofisa kilimo kata ya Iyula, Wilaya ya Mbozi, Anton Buyongera ambaye inadaiwa aliwekewa mifuko 855 ya mbolea ya ruzuku, lakini baada ya kuhojiwa alikana kupokea mifuko hiyo na wala hana shamba.

Mtuhumiwa wa tatu ni Rehema Mwandulusya, Ofisa Kilimo Kata ya Ilolo, wilayani humo ambaye anahusishwa na utoaji wa mifuko 600 ya mbolea hiyo ya ruzuku kwa kushirikiana na mtu ambaye jina lake halikutajwa kwa sababu bado anatafutwa na Jeshi la Polisi.

Mtumishi mwingine anayeshikiliwa na jeshi hilo ni James Ngunda ambaye inadaiwa kudanganya na kuwa ana shamba lenye ekari 200 na kujipatia mifuko 400.

Kaimu Kamanda Ngonyani, alisema baada ya mahojianao ya awali watuhumiwa hao wamekiri kujihusisha na wizi huo kupitia mfumo wa utoaji wa mbolea ya ruzuku.

Kukamatwa wa watumishi hao kumekuja siku chache tu baada ya Waziri wa Kilimo,Hussen Bashe kueleza kuwasiliana Mkoa wa Songwe ndio unaongoza nchini kwa kuhujumu mbolea ya ruzuku.





## Benki Exim yajitosa uhifadhi mazingira

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIKA kuunga mkono jitihada za serikali kutunza mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi, Benki ya Exim Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais wamepanda miti katika soko la Machinga jijini Dodoma.

Upandaji miti huo umeratibiwa na Taasisi ya Habari Development Association ambayo ni sehemu ya mpango wa upandaji miti 6,000 katika maeneo mbalimbali jijini hapo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupanda miti kwenye soko hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, alisema ofisi hiyo kwa kushirikiana na wadau imejipanga kuendeleza jitihada za utunzaji mazingira kwa kupanda miti katika maeneo mbalimbali nchini.

"Tukiwa kwenye mkakati huu muhimu, tunaguswa zaidi kuona kwamba wenzetu Benki ya Exim Tanzania wameamua kuungana na serikali ili kufanikisha zoezi hili muhimu.Tunawashukuru sana Exim kwa kuwa 'wanaupiga mwingi' katika jitihada mbalimbali za utunzaji mazingira hususani katika jiji hili la Dodoma," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Jafo, taifa kwa sasa linapitia vikwazo vingi vitokanavyo na athari ya mabadiliko ya tabia nchi, hivyo kusababisha upungufu wa mvua kwa karibu nusu ya kiwango kilichozoeleka.

Alisema hali hiyo imesababisha upungufu wa uzalishaji wa chakula, upatikanaji wa huduma ya maji,ukosefu wa umeme wa uhakika na hivyo kusababisha mporomoko wa uchumi.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa Exim, Shani Kinswaga, alisema benki hiyo imekuwa ikiunga mkono juhudi za serikali za kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kuja na namna mbalimbali ikiwemo kupitia Program yake ya 'Exim Go Green Initiative' kwa kuhamasisha upandaji wa miti na utunzaji mazingira nchini.

Awali Katibu Mtendaji wa Habari Development Association, Bernard Mwanawile, alisema taasisi yake imejipanga kupanda miti milioni moja mkoani hapo huku akipongeza wadau mbalimbali wanaounga mkono mpango huo ikiwemo benki ya Exim ambayo hadi sasa imefadhili upandaji wa miti 16,000.

Meneja wa Soko la Machinga, Veronica Tarimo, aliahidi kuhakikisha wataitunza vema miti hiyo sambamba na kuendelea na mkakati wao wa utunzaji mazingira.

# Serikali yatoa bil. 6/- kuboresha Mirembe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya imetumia zaidi ya Sh. bilioni sita kuboresha miundombinu katika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe jijini hapa, imeelezwa.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo jana wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu hiyo ambayo imefikia hatua za mwisho kuanza kutumiwa na wananchi kupata huduma za afya katika mazingira bora.

"Serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni sita katika kuboresha miundombinu pamoja na vifaa tiba katika hospitali hii. Sasa ni jukumu lenu watumishi kuboresha na kutoa huduma bora kwa wananchi ikiwamo matumizi ya lugha nzuri," alisema Dk. Mollel.

Pia aliiagiza Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ndani ya miezi miwili kuhakikisha inapeleka vifaa vya upasuaji wa mifupa katika hospitali hiyo ili wananchi waanze kunufaika na huduma hiyo ambayo awali walikuwa wakiifuata umbali mrefu.

"MSD leteni vifaa vya upasuaji ndani ya miezi miwili. Pia mnatakiwa kutoa kibali cha kununua dawa kwa watu binafsi kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini ndani ya saa 24, endapo dawa zinahitajika na hazipo MSD, ili kuondoa usumbufu unaoweza kuzuilika kwa wananchi," alisisitiza.

Dk. Mollel pia aliwashauri viongozi wa hospitali hiyo kuanza kufikiria namna ya kuongeza huduma zingine ili kutanua wigo wa kuwahudumia wananchi wenye uhitaji bila kuathiri huduma maalumu za magonjwa ya afya ya akili zinazotolewa katika taasisi hiyo.

Pia Naibu Waziri huyo aliagiza hospitali hiyo kupatiwa gari la kubebea wagonjwa kutokana na unyeti wa huduma zake ili kuokoa maisha ya wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

"Nawataka wakuu wa hospitali zote nchini kuacha tabia ya kuwazuia wagonjwa wa rufaa kutoka kituo kingine chochote bila kujali huduma ya mgonjwa huyo ni wa msamaha au la, hiyo itasaidia kuondoa changamoto kwa wagonjwa ikiwemo vifo vinavyoweza kuzuilika," alisema.

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Afya, Deodatha Makani, alisema wakati hospitali hiyo inaelekea kuwa taasisi, ni muhimu watumishi kujipanga na kuwahudumia wananchi kwa ubora wa juu ili kuendana na hadhi yake.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba, Wizara ya Afya, Prof. Paschal Ruggajo, alisema wakati serikali inaelekea kutekeleza sheria ya Bima ya Afya kwa Wote lazima viongozi na watumishi wajipange vizuri ili kuboresha na kutoa huduma bora kwa wananchi.



Watendaji wa Pori la Akiba la Mkungunero (waliovaa sare kushoto), wakikabidhi vifaa vya ujenzi kwa viongozi wa shule ya msingi Ihari, Kondoa, mkoani Dodoma mapema wiki hii, vilivyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), ikiwa ni sehemu ya mchango wake katika kusaidia shughuli za maendeleo ya wananchi wa vijiji jirani na pori hilo. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# RUWASA yawezeshwa kuimarisha huduma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Maji imekabidhi magari 10 kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi ili kuondoa kusuasua kwa miradi vijijini.

Magari hayo yatagawiwa katika mikoa ya Dodoma, Ruvuma, Rukwa, Morogoro, Iringa, Shinyanga, Mara , Kagera na mikoa iliyoko pembezoni mwa nchi.

Akizungumza na wandishi wa habari juzi jijini hapa wakati wa kukabidhi magari hayo, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema kero kubwa ambayo husababisha miradi kusuasua ni kutokuwapo kwa usimamizi na ufuatiliaji.

Aweso alisema kuwa serikali ilianzisha RUWASA na ndani ya muda mfupi kulikuwa na miradi kichefuchefu zaidi ya 147 lakini ndani ya muda mfupi imekwamua na kutatua kero katika miradi mingi.

"Uanzishwaji wa RUWASA lazima kuwe na vitendea kazi ili kusaidia kusimamia na kufuatilia miradi. Leo (jana) tumekabidhi magari 10 na haya ni uwezeshaji wa Rais Dk. Samia (Suluhu Hassan) na tumeshajielekeza kuwa kazi iendelee na hatuna kisingizio.

Alisema magari yatumike kwa ajili ya kusimamia miradi ya maji vijijini ili kufanikisha azma ya Rais Samia ya kumtua mama ndoo kichwani na kufikia asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini ifikapo 2025.

Aweso aliagiza RUWASA ihakikishe magari hayo yanafanya kazi iliyokusudiwa ya kusimamia miradi ya maji kwa weledi.

"Kuwapo kwa vitendea kazi hivi naamini utendaji kazi utaongezeka na kuleta mageuzi na mabadiliko makubwa kwa taasisi hii changa kuendelea kufanya kazi kubwa ya kuwasaidia wananchi kupata huduma ya maji," alisema Aweso.

Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Mhandisi Clement Kivegalo, alisema mahitaji ya magari kwa wakala ni 398 huku yalipoyopo ni 392 huku mengi yakiwa katika hali isiyoridhisha kutokana na kutumika kwa muda mrefu.

Alisema kupitia ofisi ya Waziri Mkuu, RUWASA ilipata kibali cha kununua magari 123 na kati ya hayo 38 tayari yamepatikana na yako katika mikoa mbalimbali yakiendelea kutoa huduma.

"Kibali kingine ambacho tumeshatumia ni magari 25 ambapo hayo tumeshalipia ambayo yamegharimu kiasi cha Sh. bilioni 3.8. kati ya magari hayo 10 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.5 ndio tumepokea leo na mengine 15 yatafuata," alisema Kivegalo

Mhandisi Kivegalo alimpongeza Rais Samia kwa kuwa katika kipindi kifupi ametatua kero ya usafiri kwa mamlaka ya RUWASA.

Alisema katika mwaka wa fedha ujao, serikali imeahidi kununua magari 92 ili kuendeleza kasi ya kuhakikisha wanawahudumia wananchi katika mikoa 25 wanaosimamiwa na RUWASA. Mikoa yote inahudumiwa na RUWASA isipokuwa Dar es Salaam.



# Wizara ya Afya yatambua mchango taasisi za dini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema inathamini mchango wa mashirika na taasisi za dini katika kuimarisha huduma za afya nchini.

Waziri wake, Nassor Ahmed Mazrui alitoa kauli hiyo jana ofisini kwake Mnazimmoja alipopokea msaada wa dawa mbalimbali uliotolewa na Mchungaji Mwanzilishi wa Makanisa ya Efatha Tanzania, Josephat Mwingira kwa niaba ya makanisa hayo.

Mazrui alisema wizara hiyo ina uhitaji mkubwa wa dawa kutokana na kuongezeka kwa maradhi, hivyo wanapotokea wadau na kusaidia upatikanaji wake, hupunguza mzigo kwa serikali.

"Msaada huu umekuja wakati mwafaka na tunamshukuru Mchungaji Mwingira kwa kutimiza ahadi aliyoitoa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi alipokutana naye mwezi uliopita. Ni jambo linalopaswa kupongezwa na kushukuriwa," alisema Mazrui.

Alilipongeza kanisa hilo kwa msaada huo na mingine linayoitoa kwa jamii na kuwaomba kuendelea kufanya hivyo ili kusaidia jamii ambayo ina mahitaji mengi.

Akikabidhi msaada huo kwa niaba ya Mchungaji Mwingira, Mchungaji Kiongozi wa Makanisa hayo Zanzibar, Herry Nelson alisema dawa hizo zimegharimu Sh. milioni 40 zikiwamo dawa muhimu na zinazotumika zaidi.

"Mchungaji na Mwanzilishi wa Makanisa ya Efatha, Mch. Mwingira, alipokutana na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliahidi kusaidia eneo hili na baada ya kuwasiliana na Wizara ya Afya, walituambia ni dawa gani zinahitajika zaidi na leo ndiyo tunakabidhi," alisema Mch. Nelson.

Alisema waumini wa kanisa hilo wataendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wananchi kuendeleza ustawi wa jamii kwa kukuza imani zao lakini pia misaada ya kibinadamu.

# Serikali yajizatiti utoaji wa huduma za sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango amewahakikishia wananchi serikali zote mbili zitashirikiana kukabiliana na vikwazo vilivyopo katika sekta ya afya.

Amekiri kuwa licha ya hatua ambazo serikali imepiga, bado sekta hiyo inakabiliwa vikwazo mbalimbali, ukiwamo upungufu wa vifaa tiba, uhaba wa wafanyakazi na miondombinu.

Dk. Mpango amesema serikali ipo katika hatua za mwisho kuhakikisha wananchi wanapata huduma kupitia mfuko wa huduma za afya, mpango mahususi wa kuongeza wafanyakazi katika vituo vya afya na kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinapatikana kwa wakati.

Aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa Kituo cha Afya Daraja la Pili Kendwa, Jimbo la Kiwani, Wilaya ya Mkoani, kilichojengwa kupitia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Alisema kuwa kabla ya mapinduzi, huduma za afya zikitolewa kwa matabaka kwa watu maalum huku watu wengi ambao wazawa wakiachwa na kukosa huduma.

Makamu wa Rais alisema kuwa kabla ya mapinduzi kulikuwa na vituo 44 vya kutolea huduma za afya, lakini hadi kufikia 2021 vituo vya afya vya serikali viliongezeka na kufikia 171 vikiwamo 99 vya Unguja na 72 vya Pemba.

Alisema serikali inaendelea kuweka juhudi kuimarisha huduma za kijamii kwa wananchi wake ikiwamo sekta ya afya, kwa kuwa licha ya mafanikio ambayo yapo, sekta hiyo inabaki kuwa na changamoto.

Aliwataka wanaopata fursa za kuishi katika nyumba za madaktari, kuzitunza ili kuepusha gharama za matengenezo.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh alisema malengo yao wizara ni kuhakikisha inatoa huduma bora kwa wananchi kwa kuwa tayari vifaa vimeshawekwa kwebte kituo hicho.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Massoud alizishukuru serikali kwa kuendelea kuimarisha huduma za kijamii katika mkoa huo.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Islam Seif Salim alisema kituo hicho cha afya kimegharimu zaidi ya Sh. milioni 500. Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga alisema mfuko utaendelea kuunga mkono shughuli mbalimbali za maendeleo nchini ili kupunguza changamoto zinazowakabili wananchi.



Said Mtumweni (kushoto) kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Kizimbani Zanzibar, akionyesha mche wa mti wa Mlangilangi, kwa mwananchi aliyetembelea maonyesho ya tisa ya biashara katika viwanja vya Maisara, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZMBF yaumulika ustawi wa kijamii, mazingira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mama Mariam Mwinyi amesema itaendelea kusimamia ustawi wa makundi mbalimbali ya jamii na mazingira ili kuimrisha uchumi na maendeleo ya Zanzibar.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhiwa cheti cha alama ya ubora wa taulo za kike zinazozalishwa na taasisi hiyo, katika viwanja vya maonyesho ya biashara Maisara, Mariam alisema hatua hiyo itachochea ukuaji wa uchumi.

Alisema kutokana na shughuli zinazofanywa na ZMBF, shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinaimarika hivyo kuwa na taifa lililochangamka, kuendelea na kufanya kazi na kupunguza changamoto za kijamii, ukiwamo ya umaskini.

Akizungumzia mradi wa taulo za kike zilizopatiwa alama ya ubora na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), Mama Mariam alisema umelenga kulinda afya za wasichana na wanawake, kukuza uchumi na kulinda mazingira.

"Mradi huu mbali na kuzalisha ajira, pia utasaidia katika uhifadhi wa mazingira kwa kuwa taulo hizi zinaweza kutumika zaidi ya mara moja tofauti na zile zinazotumika sasa ambazo hutupwa baada ya matumizi, hivyo kuwa chanzo cha uchafuzi wa mazingira," alifafanua.

Mama Mariam pia aliipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na ZBS kwa kuendelea kuwasaidia wafanyabishara na wajasiriamali kuzifikia ndoto za kukuza biashara na shughuli zao ili kuchangia katika uchumi wa Zanzibar.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Ali Khamis Juma alimwomba mwenyekiti huyo kuwa balozi wa kuhamasisha matumizi ya bidhaa zenye ubora na kuitangaza ZBS ili jamii izingatie ubora na viwango vya bidhaa wanazozalisha au kuingizwa nchini.

Alisema wizara imeendelea kusimamia tamasha la biashara ambalo limekua jukwaa linalowakutanisha wafanyabiashara, watoa huduma na wajasiriamali, hivyo kukuza na kuimarisha ustawi wa biashara nchini.

Akitoa taarifa ya ukaguzi wa ZBS hadi kufikia kutoa alama hiyo kwa ZMBF, Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Yusuph Majid Nassor, alisema taasisi hiyo inakusudia kuanzisha programu ya kuwasaidia wajasiriamali wanawake kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika na uendelezaji wananchi kiuchumi.

Pia aliwahakikishia wananchi na wafanyabiashara kuwa taulo zinazozalishwa na ZBMF zimekaguliwa na kuthibitishwa kuwa na ubora kwa mujibu wa viwango vya Zanzibar, Tanzania na Afrika Mashariki.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI JANUARI 14, 2023



KAJALA
Uk.13



# WEMA ANAPENDA UTUNDU

MSANII wa muziki wa BongoFleva, Whozu, amesema mpenzi wake Wema Sepetu, maarufu kama 'Chimama' ni mwanamke anayependa utanashati na utundu wa kimahaba.

Akizungumza na EATV, Whozu amesema vitu hivyo vidogo kama mwanaume hana vinamk-waza, na yeye vigezo anavyo ndio maana anadumu naye mpaka sasa.

"Wema huwa hapendi uchafu anapenda mwanaume msafi na mtundu na ndio maana ananipenda na mimi nampenda," amesema Whozu.

Amesema uhusiano wao utazidi kuimarika mwaka huu baada ya kufunga ndoa.

Whozu ameongeza kwamba suala la dini kwao si tatizo kwani hata yeye yupo tayari kubadili dini ili suala la ndoa lifanyike haraka.

Akizungumzia kuongezeka mwili wake kwa haraka, amesema inatokana na aina ya vyakula anavyopikiwa na Wema, ambaye ni mtaalamu wa mapishi.

"Mwili wangu unaongezeka kutokana na vyakula vitamu ninavyopikiwa na mpenzi wangu, si mnajua jinsi alivy-okuwa mtaalamu wa mapishi? Msiniulize kwa sababu jibu mnalo," ameongeza kusema.

BASI SAWA

# Baby Madaha afurahia ndoa




MWANAMUZIKI Baby Madaha, amesema mwanaume aliyekuwa akimtafuta muda mrefu kuwa mume wake sasa amempata, hawezi kwenda kudanga kutafuta pesa.

Amesema alikuwa anataka mume ambaye sio staa na mwenye pesa kiasi, na ndivyo mume wake anazo sifa hizo.

Amesema kutokana na maisha yake ya ndoa, mume wake amemfanya kuwajibika zaidi kwa jamii, kiasi ambacho amemtengeneza kuongoza taasisi isiyo ya kiserikali.

"Suala la muziki na filamu kwa sasa nimeweka kando kidogo nafanya kazi za kijamii nikisaidiana na mume wangu,"

# Bahati Music aileta 'We Next Records'



UKUAJI wa kasi wa muziki wa Bongo Fleva, unazidi kuwavutia wamiliki wa lebo mbalimbali ambao wana nia ya kuwekeza nchini.

Mtayarishaji wa muziki anayeishi Marekani, kutoka lebo ya 'We Next Records', Bahati Music amesema ana lengo la kufungua ofisi nchini kama njia ya kuinua vipaji vya Afrika.

Akizungumza na BT, Bahati Music ambaye yupo Bongo kwa sasa, amesema studio hizo za audio na video zimeshaanza kufanya kazi na wasanii mbalimbali wa Tanzania.

"Ili tuweze kuifikia Tanzania na Afrika kwa ujumla tumefungua studio zetu Sinza Kumekucha na tayari tumeanza kufanya kazi chini ya mtayarishaji Adventure, haya ni mapinduzi makubwa mwaka huu kwenye tasnia ya muziki," amesema Bahati.



# Gloria awakumbusha 'Maisha' yana mwisho

MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi katika muziki wa Injili, Gloria Mwasambili, ameanza mwaka 2023 kwa kutambulisha kibao chake kipya 'Maisha' ambacho kitaleta ushindani kwa wasanii wakongwe.

Akizungumza na BT, Gloria, amesema lengo la kutoa wimbo huo ni kuwakumbusha watu kwamba maisha ni mafupi sana hapa duniani, hivyo wakumbuke kuna kifo na huwezi kujua lini utaondoka.

"Nataka kuwakumbusha watu kwamba wakati tunafurahia dunia, tukumbuke siku moja tutakufa na hivyo tufanye mambo mema yanayompendezesha Mungu," amesema.

Amesema ameachia wimbo huo kwa njia ya Audio, wakati yupo katika harakati za kukamilisha video.

Pamoja na uimbaji Gloria ni hakimu wa mahakama ya mwanzo Kelege wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani





# Kajala kawapa watu maswali

KAULI ya Staa wa filamu nchini Kajala Masanja kuwa ana mpango wa kuzaa mtoto mwingine wa pili imeibua maoni tofauti.

Hivi karibuni Kajala ameshea matamanio yake ya kutaka kuwa mama tena na kupata mdogo wake Paula.

Wafuasi wake walioshiriki maoni yao, kila mmoja alionekana kuwa tofauti, kuna wale walimpongeza na kumtaka kutekeleza mpango huo haraka na wapo waliomwambia kwa sasa apumzike kutokana na umri wake kuwa mkubwa.

# Machawa wa 5 mastaa Bongo

**Na Adam Fungamwango**

KILA kukicha mambo yanaongezeka, na kila siku yanazuka mapya. Nchi hii siku hizi mchawi bando tu, ukiwa nalo utasikia mengi.

Kuna kazi ambayo imezuka siku hizi inaitwa uchawa. Kabla hatujaenda mbali hebu tuangalie chawa ni nini?

Chawa ni wadudu wadogo, ambao wako wa aina mbili. Kuna wanaokula nywele, manyoya na seli za ngozi zilizokufa, na wanaofyonza damu ya mwenyeji wao. Chawa wa aina ya kwanza wana vipande vya mdomo vya kutafuna, wale wengine wana mdomo wa kufyonza. Miguu inabeba aina za maganda madogo ili kushika nywele au manyoya ya mwenyeji. Kwa kawaida mayai ya chawa yanagandia nywele au manyoya.

Siku hizi kuna machawa watu. Wamepewa jina hilo kwa sababu ya kuwa na sifa kama chawa wadudu, nayo ni kuwaganda mabosi wao.

Kwa tafsiri ya wengi mitaani ni kwamba chawa ni mtu anayejipendekeza kwa mtu mwenye pesa au maarufu ili anunuliwe vitu vidogovidogo au naye apate umaarufu.

Machawa watu wale wanamshangilia, kumtetea, kumshauri na kumtia nguvu mtu yeyote wanaemsapoti. Hawa wapo tayari kugombana, kumsema au kupambana na mtu yeyote ambaye anamshambulia kwa maneno au kumsema vibaya mtu wanaemsapoti.

Mara nyingi watu hao huwa ni wanamuziki, wasanii, wafanyabiashara au baadhi ya watu wengine maarufu, ambao wanakuwa na watu wa aina hiyo ambao ni kama vile wapambe wake.

Hawa machawa wamezidi hata wapambe. Inasemekana hapa Bongo machawa hufanya kazi hii kwa mambo mawili. Kulipwa, pamoja na kujipatia umaarufu ili na wao wafanye mambo yao. Hapa mjini ukishakuwa maarufu unaweza kufanya biashara ya shughuli nyingine halali ya kujipatia kipato mambo yakakuendea. Ukiwa karibu na waridi unanukia. Ukiwa chawa wa mwanamuziki maarufu na wewe pia utakuwa maarufu.

Inasemekana kuna wanaolipwa ujira na wanaridhika tu, lakini wengine hujiongeza kwa kujiongezea umaarufu ili 'kujibrandi'.

Ndiyo maana wakati mwingine utaona ajabu chawa wa huyu anahama, anakwenda kwa mwingine.

Sifa zote alizokuwa akizitoa kwa huyu na kumponda yule, leo zimegeuka anaanza kumponda bosi wake wa zamani.

Wapo wengi sana, lakini leo tuangalie machawa watano ambao wamekuwa maarufu sana nchini. Yaani hawa ukimtaja tu kila mmoja atakwambia huyu ni 'chawa'.

**MWIJAKU**

Huyu ni mwigizaji na mtangazaji, ambaye awali alikuwa chawa wa msanii Harmonize, lakini kwa sasa amegeuka na kuwa chawa wa kutupwa wa hasimu wake, Diamond Platnumz.

**BABA LEVO**

Jamaa ni msanii wa muziki wa bongo fleva, huyu ni chawa wa kugalagala wa Diamond Platnumz.

**ARISTOTE**

Huyu ni chawa na wasanii kama Diamond Platnumz, Irene Uwoya na baadhi ya wafanyabiashara maarufu nchini. Hutumia kazi hiyo na yeye mwenyewe 'kujibrandi' ili kujiongeza umaarufu ambao humpatia dili mbalimbali na si kutegemea tu pesa za kupewa peke yake.

**H BABA**

Ni msanii maarufu tu, lakini kwa sasa naye ni chawa wa Diamond, humuelezi lolote kwa msanii huyo ambaye kwa hapa tu inaonyesha ndiye anayeongoza kuwa na machawa wengi mastaa.

**JUMA LOKOLE**

Ni mtangazaji, mshereheshaji, lakini ni chawa wa msanii Diamond Platnumz.



MWIJAKU




# Mapenzi yamekufa: kizunguzungu kisichoisha

**Na Adam Fungamwango**

MAPENZI hayako sahihi kabisa. Mapenzi huwa hayajulikani yanataka nini. Mapenzi hutaka yanavyotaka yenyewe siyo anavyotaka mpendaji au mpendwaji. Mapenzi ni kigeugeu, leo hivi kesho vile.

Haya ndiyo mapenzi jinsi yalivyo, hayana shule, wala bingwa. Hajawahi kutokea bingwa wa mapenzi duniani.

Tutazunguka kote, lakini hebu tuangalie filamu hii iitwayo 'Mapenzi Yamekufa'. Hata tutaona kizungumkuti kuhusu mapenzi.

Msondo wameshawahi kuimba kuwa, huku kuna harusi, mtaa wa pili kuna mtu kajinyonga kwa ajili ya mapenzi na wala si ajabu masikini kupendwa na tajiri kukimbiwa.

Imechezwa na wasanii Magoma Moto, Anneth James, Asha Khamis, Akida Juma, Mariam Ally na wengineo.

Mosi na Magoma ni mtu na mpenzi wake. Kwa upande wa pili Mazembe na Sima pia ni mtu na mpenzi wake. Hawa wote wanafahamiana.

Hawa mademu kumbe rohoni kila mtu ana lake. Mosi ambaye mpenzi wake Magoma ana uwezo, anampenda Kazembe japo ni masikini.

Halafu Sima yeye anajigonga kwa Magoma Moto kwa sababu ana uwezo. Wote wakawa wanaibana.

Siku isiyo na jina wanafumananiana, na kila mmoja sasa anabaki na demu wa mwenzake.

Magoma akawa na Sima, Kazembe yeye akabaki na Mosi. Baada ya wiki moja, Mosi akaondoka kwa Kazembe kurudi kwa bwana yake wa zamani Magoma. Akamkuta Sima amejaa tele kama pishi ya mchele. Wivu ukamshika. Akadhamiria kwenda kujiua porini. Aliokolewa na jamaa mmoja mlevi aitwaye Bondo. Ikabidi aishi kwa muda kwa mlevi huyo chini ya uangalizi kwa sababu hakuwa sawa kisaikokojia.

Sima naye akatoka kwa Magoma akaenda kwa Kazembe. Akamwambia japo wameachana kwa kufumaniana, lakini ana ujauzito wake, lakini asithubutu kusema. Amembambikia Magoma kwa sababu ana pesa.

Anarudi tena kwa Magoma kuendelea na maisha yao. Magoma anatembelewa na kaka yake Chenada. Anapomuona Sima yupo pale anashangaa. Kumbe walishawahi kuwa wapenzi huko nyuma, baada ya siku mbili tatu, Sima anamwambia kuwa iwe siri yake, asimwambie mdogo wake kuwa walishawahi kuwa wapenzi huko nyuma.

Chanada anamwambia kama akitaka iwe siri basi wawe wapenzi wa kisirisiri mdogo mtu asijue.

Mosi naye baada ya kuokolewa na mlevi akikaa kwa siku kadhaa akaamua arejee kwa Kazembe. Alipofika alimkuta mwanamke mwingine.

# Nkiru hata ndoa inatangazwa



Mwigizaji wa Nollywood, Nkiru Sylvanus, yuko katika hatua ya mwisho ya kufunga ndoa.

Msanii huyo ameshirikisha kwenye ukurasa wake wa Instagram, picha ambayo inaonekana imepigwa kabla ya harusi kwenye Instagram leo,

Mwigizaji huyo hakuonyesha sura ya mume wake mtarajiwa, lakini alionyesha mgongo wake, mkono na sehemu zingine ambazo hazikutoa utambulisho wake.

Mnamo Desemba 30, 2022, mwigizaji huyo alitangaza kuwa alikuwa amechumbiwa.



## Mungu kamnusuru na balaa

MTAYARISHAJI wa muziki maarufu nchini Nigeria, Magicstics, amenusurika kifo baada ya kupata ajali ya gari.

Magicstics ambaye anatamba na ngoma nyingi katika lebo ya Asake, ameeleza kuwa yeye na mama yake walipata ajali mbaya na kunusurika kwa mapenzi ya Mungu pekee.

Alifichua kuwa ilikuwa kawaida yake kusherehekea Mwaka Mpya na mama yake, na alipokuwa akitoka naye, walipata ajali wakati tairi moja ya gari yao ilipasuka wakati wakishuka mlimani.

## Ay mbona hao wapo wengi tu

MCHEKESHAJI, mtayarishaji wa filamu na mwigizaji kutoka Nigeria, Ayo Makun, maarufu kwa jina la AY, ametoa ushauri mzito kwa wasanii wenzake katika tasnia ya burudani.

AY aliwashauri kuacha kutafuta uthibitisho kutoka kwa watumiaji wa mtandao, na kwamba ukweli au uwongo hautawafanya watu wawapende.

Aliwaomba kujinusuru na msongo wa mawazo na kulinda afya zao za kiakili.





## Kylie, Scott waachana tena

MWANAMITINDO na mjasiriamali, Kylie Jenner na mume wake Travis Scott wameripotiwa kuachana tena baada ya kurudiana mnamo 2020.

Fox News imeripoti kwamba wanandoa hao walitumia Krismasi wakiwa wametengana, na Kylie alikuwa Aspen na binti yao wa miaka minne Stormi Webster.


"Kylie na Travis wameachana tena; walipaswa kutumia likizo pamoja, lakini Kylie alienda Aspen kuwa na familia yake na marafiki huko,"kilisema chanzo kimoja.

## Burna Boy kafa kwa mrembo mjeshi

MWIMBAJI wa muziki wa Afrobeat kutoka Nigeria, Burna Boy, ameshindwa kuhimili moyo wake, baada ya kueleza alijikuta akiganda kwa muda baada ya kumuona mwanamke mrembo mwanajeshi.

Mshindi huyo wa tuzo ya Grammy, ameandika katika ukurasa wake wa Instagram kuwa alikutana na mwanamke huyo mitaani na akiwa amevaa sare za jeshi, lakini alishindwa kumsogelea kutokana na kupata hofu.

Kulingana na Burna Boy, hakuwa na maneno sahihi ya kumuelezea mwanamke huyo, akisema ni mrembo sana japokuwa ni mwanajeshi.





# Aliyeuawa madai kumtusi mamaye azikwa Sanawari

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKAZI wa wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Nelson Mollel (32), aliyefariki dunia juzi baada ya kuchapwa fimbo 280 kwa sheria za kimila, akituhumiwa kumtusi mama yake mzazi, alizikwa jana nyumbani kwao, Sanawari.

Akizungumza na Nipashe jana, dada wa marehemu, Jackline Mollel, alisema mdogo wake atapumzishwa kwenye makaburi ya nyumbani kwao baada ya taratibu zote za maziko yake kukamilika.

"Hakika inauma sana kwa mazingira ya kifo hiki kilichotokea marehemu tutampumzisha kwenye nyumba yake ya milele leo hapa hapa nyumbani,"alisema.

Wakati familia ikiwa imeamua kumzika Nelson baada ya mvutano, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema makachero wa jeshi hilo wanaendelea na msako wa kutafuta wahusika wa tukio hilo, akiwamo baba mdogo wa marehemu anayetuhumiwa kuongoza ukatili huo.

Juzi, Jackline alinukuliwa na Nipashe akisema mdogo wake alikutwa na mauti, baada ya kuchapwa fimbo 280 badala ya fimbo 70 zinazotakiwa kuchapwa kwa mujibu wa mila na desturi za mila ya kabila la Kimasai.

"Lakini baada ya kumchapa fimbo hizi 280, walimwagia tindikali eneo la kiunoni na kupoteza maisha. Mila zetu zinataka mtu mwenye utovu wa nidhamu, achapwe fimbo 70 lakini wao walipitiliza," alisema.

Dada wa marehemu alisema hawakatai wala hawapingi adhabu aliyopewa mdogo wao na baba yao mdogo, aitwaye Abel Mboya, kwa kushirikiana na watu wengine 10, kumchapa fimbo hizo bila kuangalia afya ya mhusika huyo.

"Sisi hatukatai ndugu yetu kuchapwa, maana ni mila na desturi zetu sisi Wamasai, lakini wamezidisha na wamemchapa kwa sifa na wamemvunja mbavu, miguu, mikono na kumwagia tindikali chini ya kiuno," alisema.

Akizungumzia tukio hilo, mama mzazi wa marehemu aitwaye Janeth Kimario, alikiri ni kweli marehemu, ambaye ni mwanae alimtukana matusi hayo ya nguoni, Januari mosi mwaka huu.

"Baada ya kunitukana, nilimwambia baba yake mdogo, Abel Mboya (45), ambaye alimwita na kumpeleka porini, na nikajua anamchapa fimbo 70 ambazo mila zetu zinataka.

"Adhabu aliyopewa mwanangu ni kubwa, japo alistahili kuchapwa kufundishwa adabu, lakini hata hivyo, hawakunimbia kama watampa adhabu kubwa hivyo hadi kupoteza maisha," alisema.

# Kiu ya wakulima kuhusu mbolea yapungua

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

HATIMAYE Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) na Kampuni ya SBL ya Kenya, zimejibu kiu ya muda mrefu ya wakulima waliokuwa wakitafuta mbadala wa mbolea za kemikali.

Hatua hiyo ni baada ya kuingiza toleo jipya la mbolea ya asili ambayo ni rafiki wa mazingira.

Licha ya kuwa rafiki wa mazingira, hurutubisha udongo na kuhifadhi unyevunyevu kwenye shina la mmea. Mbolea hiyo inatajwa kupunguza gharama kubwa za uzalishaji kwa mkulima na kumpa tija mwisho wa mavuno.

Akizungumza jana jijini Arusha na mawakala wa pembejeo za kilimo wakati wa uzinduzi wa mbolea hiyo kwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga, Meneja wa TFC Kanda ya Kaskazini, Cosmas Ngh'oboko, alisema mbolea hiyo inauzwa kwa bei rahisi zaidi ya mbolea zingine.

"Mbolea hii hivi sasa inapatikana kwenye vituo vyetu, mfuko mmoja ambao ni wa kilogramu 25, utauzwa kwa Sh.30, 000 na wa kilogramu 50 utauzwa kwa Sh. 60,000.

"Pamoja na kwamba kuna mbolea ya ruzuku, ambayo inaendelea kutolewa kwa sasa, lakini pia tutaenda pamoja sambamba na hii mbolea ambayo na yenyewe haitakuwa kwenye ruzuku," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya SBL inayozalisha mbolea hiyo nchini Kenya, Joel Kariuki, alisema kinachofanyika kwa sasa ni matokeo ya makubaliano yaliyofikiwa kati ya Rais Samia Suluhu Hassan (Tanzania) na William Ruto (Kenya) ya kuondoa vikwazo 14 vya kibiashara vilivyokuwa vikidhoofisha ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi katika mataifa hayo mawili.

Aidha, Kariuki alisema kampuni hiyo imelenga kuwainua wakulima wa Tanzania, kwa kuwauzia mbolea hiyo kwa gharama nafuu ili kupunguza gharama za uzalishaji.

"Tumekuja hapa Arusha kutekeleza makubaliano ya Rais wa Kenya na Rais wa Tanzania, kufungua mipaka ya biashara, waone vile tunafanya biashara. Tunawashukuru marais hawa, sasa tunafanya vizuri na tumeanzisha ubia.

"Sasa hivi tumeleta mbolea yetu mpya Arusha, Manyara na Moshi na kwingine. Makubaliano ya marais hawa, yametusaidia kufanya biashara kwa uwazi bila kusumbuliwa Afrika Mashariki," alisema.

Katika uzinduzi huo, Katibu wa Chama cha Mawakala wa Pembejeo za Kilimo wa Mkoa wa Arusha, Humphrey Msuya, alisema mbolea hiyo imekuja kama suluhisho kubwa kwa tatizo lililokuwa linawakabili wakulima wa Tanzania.

"Kwa muda mrefu tumekuwa na mahangaiko ya kutumia aina mbalimbali za mbolea, ambazo ni hizi za kemikali.

"Mara nyingi mbolea za kemikali inaaminika zinaharibu udongo, kwamba zinaenda kulenga kuustawisha mmea, lakini hazijali udongo ambao ndio asili ya ule mmea. Na katika kufanya kwangu biashara za pembeo za kilimo Arusha na kule Manyara, wao mbolea za kemikali walikuwa wanazikataa kabisa, wakiamini kwamba zinaharibu udongo," alisema.

Alisema ujio wa mbolea hiyo unalenga zaidi kuwasaidia wakulima kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao yao na kuwasogeza kiuchumi kutokana na nafuu ya mbolea.



Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Misaile Musa, akizungumza wakati akiwakaribisha Maofisa Elimu Sekondari na Msingi pamoja na baadhi ya wakuu wa shule, walioongozwa na Ofisa Elimu Mkoa wa Kagera, waliofika mkoani humo jana, kwa ziara ya mafunzo kuhusu mafanikio ya kielimu yaliyofikiwa na mkoa huo kwa kuwa ni moja kati ya mikoa bora inayofanya vizuri katika ufaulu wa mitihani ya shule za sekondari na msingi kwa miaka mingi mfululizo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# TAMIDA yafichua njama utoroshaji madini

**Na Asraji Mvungi,** SIMANJIRO

CHAMA cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (TAMIDA), kimeiuma sikio serikali, kikiitaka kutumia taasisi zake kufuatilia na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya taarifa zinazotolewa na baadhi ya watu wasio na nia njema za kuwapo kwa mianya ya utoroshaji madini ya tanzanite.

Katika ushauri wake alioutoa kwa Wizara ya Madini Mwenyekiti wa TAMIDA, Sammy Mollel, amesema licha ya taarifa zinazotolewa kuonyesha wazi kuwa ni za upotoshaji, ni vizuri wanaohusika wakachukuliwa hatua kali, kwa kuwa kuendelea kufumbia macho, kunadumaza soko la madini hayo kitaifa na kimataifa.

Mollel alikuwa akizungumza jana na wadau wa madini na viongozi wa serikali, baada ya kutembelea na kukagua migodi hiyo iliyoko eneo la Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara.

"Licha ya kuwapo kwa udhibiti mkubwa katika uchimbaji na uuzaji wa rasilimali hiyo, bado upotoshaji ni mkubwa na ni hatari kwa soko la madini. Kama wadau tunasikitishwa na taarifa hizo. Niwaombe sana Watanzania tutoe ushirikiano wa kuwabaini watu hao na kuwataja hadharani, na pia kama yupo mwenye taarifa za ukweli wa jambo hilo, basi azitoe ili hatua ziweze kuchukuliwa.

"Tangu kujengwa kwa ukuta katika eneo hili mwaka 2017 na kufungwa kwa mitambo ya kielektroniki ya ulinzi, kumesaidia sana kuondoa mianya ya utoroshaji wa madini.

"Kwa hali inayoonekana kwa macho, sio rahisi madini kutoroshwa kutokana na udhibiti mkubwa uliopo. Taasisi zote za serikali zipo, mifumo yote imekamilika na inafanya kazi, huo utoroshaji unaodaiwa unafanyika, je ni kwa njia gani? alihoji Mollel.

Akiunga mkono hoja hiyo ya TAMIDA, Ofisa Madini Mkazi katika machimbo hayo ya Mirerani, Menard Msengi, alisema serikali imeweka ulinzi wa kutosha na mazingira mazuri, kuanzia kwenye miradi hadi kufikia sokoni, hivyo si rahisi kuwapo utoroshaji unaotajwa.

Aidha, Mwenyekiti wa Chama cha Wanunuzi Wadogo wa Madini Tanzania (CHAMATA), Jeremia Kituyo, akizungumza katika kikao hicho, alisema taarifa za kuwepo kwa utoroshaji wa madini zinasababisha washindwe kufanya biashara, kwa sababu zinawaondolea uaminifu kwa wateja wao.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# 'Rice cooker' ilivyoua utamu wali uliopaliliwa na mkaa

**Na Adam Fungamwango**

TEKNOLOJIA licha ya kwamba imeleta maendelea makubwa sana na kurahisisha maisha, lakini imekuja kuondoa baadhi ya vitu vya kitamaduni.

Huko nyuma tuliwahi kuelezea jinsi teknolojia ilivyorahisisha kizazi cha sasa kupata wapenzi na wake kwa urahisi, tofauti na zamani ambapo hakukuwa na simu za mkononi kiasi kwamba watu waliganda sana kwenye vituo vya basi, au sehemu walizoahidiana wapenzi, na kule vijijini ilikuwa tafrani tupu, kwani watu waligandishwa kwenye miti, vichaka, huku wakiwa hawana uhakika wa wapenzi wao kuja, kwa kuwa tu hakukuwa na mawasiliano.

Vile visa vilivyokuwa vikitokea kutokana na kutokuwa na teknolojia ilikuwa ni burudani tosha.

Leo tunaangalia teknolojia kwenye mapishi. Imekuja kurahisisha chakula kuiva kwa muda mfupi kwa kutumia jiko la gesi na umeme, bila mpishi kuhangaika sana au kuchafuka.

Zamani ili kupika chakula lazima kwanza vitafutwe vifuu kwa wakazi wa mikoa wa Pwani, ukanunuliwe mkaa, au liwashwe jiko la mchina, na jiko lililoonekana ni la kisasa zaidi na linaloivisha kwa haraka zaidi, stovu.

Hiyo ndiyo faida ya teknolojia, lakini bado kuna watu wanadai baadhi ya vyakula havinogi vikipikwa kisasa.

Wanakumbuka miaka ya 1990 kurudi nyuma, wakati kinadada na kinamama walivyokuwa wakipika wali kwa kutumia mkaa, vifuu au kuni.

Halafu baada ya kuiva, sufuria la watu linafunikwa juu. Ule moto wa mkaa, kuni au vifuu unagawanywa. Nusu unabakishwa kwenye jiko au mafiga, halafu mwingine unawekwa juu ya mfuniko.

Kwa lugha rahisi iliyokuwa inatumika wakati ule na nadhani hata sasa ni kupalilia.

Baada ya hapo utaachwa hapo na nadhani baada ya masaa mawili hivi, utapakuliwa, tayari kwa ajili ya chakula cha familia.

Wali huo utiwe na nazi au mafuta ulikuwa unanukia vizuri, kwa sababu tayari juu wali unakuwa umeungua na kutengeneza kitu kama utandu hivi na jina lake linaitwa matandu, wengine huita mahaba, ili mradi kila mtu na jina lake.

Upishi wa aina hiyo ulitengeneza matandu, halafu chini ukatengeneza kitu kinaitwa ukoko.

Matandu na ukoko ulikuwa ndiyo vipenzi vya watoto wa zamani. Na wengi wao walipenda mno wali na maharage. Wenyewe waliita ubwabwa na maharage. Watoto wa zamani hawakuwa na makuu. Hakuhitaji wali kuku, wali nyama, wali samaki wala nini. Wao ni wali na maharage tu.

Sasa ndiyo ilkute wali ulioungwa na nazi umepaliliwa na maharage nayo yaungwe na nazi. Ni hatari tupu.

Sasa burudani inaanza pale akinamama wanapoanza kupika wali huo. Watoto siku hiyo hawaendi kucheza mbali. Ikumbukwe kuna miaka hasa mwishoni mwa 1970 hadi miwshoni mwa 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990, mchele ilikuwa



bidhaa adimu sana nchini Tanzania. Siku ikipikwa nyumbani, balaa lake linakuwa kubwa.

Wengine wanajifanya wanasinzia ili upakuliwe mapema, lakini akishakula wanaenda kucheza. Hakuna tena usingizi. Wengine hata wale ambao ni wabishi kuoga, siku hiyo bila fimbo wala kulazimishwa wanaoga mapema. Kisa siku hiyo unapikwa ubwabwa nyumbani.

Mama atapalilia na wakati wa kupakua, watoto wataanza kupewa matandu kwanza, kabla ya ubwabwa.

Halafu kesho yake asubuhi, watoto huamka mapema hata kama si siku za kwenda shule. Kisa ni kwamba wanakumbuka kuwa jana ulipikwa ubwabwa, lengo ni kutaka wapakuliwe ukoko ambao unamiminiwa na mchuzi mwingi wa maharage.

Hapo watoto wataanza kula ukoko kwanza, kabla ya kula ubwabwa na chai asubuhi.

Ukimuuliza mtoto yoyote wa miaka hiyo, atakwambia utamu wa matandu na ukoko, jinsi mapishi ya akinamama wa wakati huo kutokana na kupika kwa kutumia mkaa, kuni na hata vifuu.

Kutokana na kukua kwa teknolojia, hivi sasa kwa asilimia 90, hasa wakati za mijini hawatumii sana mkaa, vifuu wala kuni.

Angalau vijijini, ambako bado kuna kuni ambazo wanatumia. Lakini vile vile wanawake wengi kwa sasa wamekuwa hawatumii tena aina ya mapishi ya kupalilia wali, labda wale wa mikoa ya Pwani kama vile Tanga, Lindi na Pwani yenyewe hasa Bagamoyo.

Ni aghalabu sana leo kukuta wali unapaliliwa kutokana na teknolojia, kwani sasa wengi wanatumia 'rice cooker' na hata jiko la gesi kupika wali, hivyo haiwezekani.

Ukipika kwa njia hiyo huwezi kupata matandu wala ukoko chini. Ndiyo maana wengi waliozungumzia hili ambao ni watu wazima, walionekana kukumbuka sana matandu na ukoko, lakini kwa sasa wakadai hawawezi kuupata kwa sababu wake zao ni wa kisasa, na wanatumia majiko ya kisasa.

Wengi walikuwa wanakula matandu na ukoko kwa mapishi waliokuwa wakipika mama zao enzi hizo. Kwa sasa wanabaki na kumbukumbu tu na kusimulia tu, lakini ni nadra sana kuupata wali wa kupaliliwa, ambao ulikuwa mtamu na wenye kunukia.

Watoto wa kizazi cha sasa wao ndiyo kabisa. Wao ni kwenye 'rice cooker' na jiko la gesi tu.

Ukiwasimulia mambo ya wali wa kupaliliwa, matandu na ukoko, watakushangaa tu.

**Tuma meseji 0716 350534**






# Ufaransa, Ujerumani zahimiza uwajibikaji

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

MAWAZIRI wa mambo ya kigeni wa Ufaransa na Ujerumani, wameitumia ziara yao ya siku mbili nchini Ethiopia kutoa wito wa uwajibikaji kwa matukio ya unyanyasaji yaliyofanywa wakati wa mzozo wa Tigray.

Viongozi hao walisema utekelezaji huo ni kama sharti la Umoja wa Ulaya kurejesha mahusiano na nchi hiyo. Akizungumza mjini Addis Ababa, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ujerumani, Annalena Baerbock, alielezea kuwepo kwa uhalifu ukiwemo unyanyasaji wa kingono wa kimfumo, uliofanywa wakati wa vita hivyo vya miaka miwili na nusu na maelfu ya watu wanadhaniwa kufa.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ufaransa Catherine Colonna, alisema utekelezwaji wa muafaka wa amani uliotiwa saini kati ya waasi wa Tigray na serikali ya shirikisho la Ethiopia na kutimiza ahadi za uwajibikaji ndio sharti la kurejesha mahusiano na Ulaya.

**DW**

# Sweden yagundua hifadhi ya madini

**STOCKHOLM,** SWEDEN

SWEDENI imegundua hifadhi kubwa ya madini adimu ya chuma yenye thamani na ambayo yanahitajika duniani.

Miongoni mwa mambo ambayo madini hayo yanatumika ni ujenzi wa magari ya umeme na mitambo ya kuzalisha nishati ya upepo.

Kampuni ya madini ya Sweden (LKAB), imetangaza kuwa zaidi ya tani milioni moja ya madini hayo ya nadra ya chuma imepatikana karibu na eneo la Kiruna, ikiwa ni hifadhi kubwa ya madini hayo kuwahi kugundulika barani Ulaya.

Mkuu wa kampuni ya LKAB, Jan Mostrom, alisema madini hayo huenda yakaimarisha uzalishaji wa malighafi ambayo ni muhimu katika kuhamia kwenye nishati mbadala.

Mastrom alisema ni vigumu kukadiria ukubwa wa hifadhi hiyo ya madini hayo ya nadra ya chuma ikilinganishwa na nyingine za nje ya Ulaya.

# Russia yadhibiti Soledar, vikosi vyauzingira Bakhmut

**MOSCOW,** RUSSIA

RUSSIA imesema imeudhibiti mji wa mgodi wa chumvi nchini Ukraine wa Soledar, baada ya mapigano makali na kutaja kuwa ni hatua muhimu.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, imesema ushindi huo utaruhusu wanajeshi wake kuvikata vikosi vya Ukraine katika mji mkubwa wa Bakhmut.

Hapo awali, Ukraine ilisema vikosi vyake bado vinapigana na kwamba kumekuwa na mapigano makali usiku kucha.

Mapigano karibu na Soledar yamekuwa vita vikali vyenye umwagikaji wa damu tangu mzozo huo kuanza.

Naibu Waziri wa Ulinzi wa Ukraine, Hanna Malyar, alisema jana kwamba mapigano yalikuwa yakiendelea na kwamba kulikuwa na moto huko Soledar usiku kucha. Wapiganaji wa Ukraine walikuwa wanajaribu kwa ujasiri kushikilia ulinzi.

Umuhimu wa mji huo kwa jeshi la Russia unapingwa na wachambuzi wa kijeshi, lakini kutwaa Soledar kunaweza kusifiwa kama ushindi baada ya miezi kadhaa ya kushindwa katika vita vya miezi 10.

Taasisi ya Utafiti wa Vita yenye makao yake makuu nchini Marekani, ilisema saa chache mapema kwamba kuna uwezekano kwamba vikosi vya Russia viliiteka Soledar, lakini haikuamini kuwa inamaanisha kwamba wangeweza kuzunguka Bakhmut.

Hata hivyo, Ukraine imepinga ushindi huo na kueleza wanajeshi wake wanaendelea kupambana katika mji wa mashariki wa Soledar baada ya usiku wenye mapigano makali.

Pande zote zimekumbwa na hasara katika mapambano ya kuwania udhibiti wa mji huo mdogo.

Ukraine ilisema Russia inaendelea kupeleka vikosi vingine vya wanajeshi katika eneo hilo la Soledar, maarufu kwa uchimbaji chumvi.

Soledar ipo katika mkoa wa kiviwanda wa Donestk ambao Russia inalenga kuukamata.

Naibu Waziri wa Ulinzi wa Ukraine, Hanna Malyar, alisema ilikuwa ni usiku wa moto katika eneo la Soledar ambako mapambano yanaendelea, akiita hii kuwa awamu ngumu ya vita hivyo lakini mwishowe watashinda.

Wakati huo huo, Rais wa Ukraine, Zelensky katika mtandao wake wa twitter, alisema amezungumza na Rais wa Kenya, Willium Ruto, kuhusu usalama wa chakula.

Rais Zelensky alisema pia walizungumza kuhusu kuundwa kwa hifadhi za nafaka barani Afrika, na kukubaliana kuimarisha ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.

Rais wa Ukraine pia alishukuru Kenya kwa msaada wake na ushirikiano wa kujenga katika Umoja wa Mataifa katika vita nchini mwake dhidi ya Russia.

Ofisi ya rais wa Kenya haijatoa tamko lolote kuhusiana na mazungumzo hayo.

Kenya ilipinga uvamizi wa Russia katika hotuba iliyowasilishwa kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mara baada ya vita kuanza.

Rais Ruto alisema amejitolea kutekeleza jukumu kuu la ushirikiano katika ngazi ya kimataifa katika kutatua mgogoro wa Ukraine.

**BBC**



Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Qin Gang (kulia) akisalimiana na mwenzake wa Ethiopia, Demeke Mekonnen, wakati wa ziara yake nchini Ethiopia juzi. **PICHA: ANADOLU AGENC**

# Rais Biden kuchunguzwa kukutwa na nyaraka za siri

**WASHINGTON**, MAREKANI

MWANASHERIA Mkuu wa Marekani, Merrick Garland, amemteua mwanasheria maalum kuchunguza jinsi Rais Joe Biden alivyoshughulikia nyaraka za siri.

Robert Hur, ofisa mkuu wa zamani wa idara ya haki wakati wa urais wa Trump, ataongoza uchunguzi huo.

Nyaraka zilizopatikana hivi majuzi zilikutwa nyumbani kwa Biden na katika ofisi aliyotumia baada ya muda wake kama makamu wa rais kumalizika.

Ikulu ya White House ilisema Rais Biden, atashirikiana kikamilifu na uchunguzi huo.

Kupatikana kwa nyaraka hizo kunaonekana suala la aibu kisiasa, kwani inakuja wakati wa uchunguzi unaoendelea kuhusu madai ya Rais wa zamani Donald Trump na yeye kukutwa na nyaraka zingine za siri.

Kundi la kwanza la nyaraka hizo lilipatikana Novemba 2, katika ofisi ya Penn Biden, iliyoko huko Washington DC, na kukabidhiwa kwa Hifadhi ya Kitaifa ya Marekani.

Garland alisema kundi la pili la nyaraka hizo zilibainika Desemba 20, nyumbani kwa Biden huko Wilmington, Delaware.

Aliongeza kuwa Alhamisi asubuhi, mawakili wa Biden waliwaita wachunguzi kuwaarifu k uhusu nyaraka za ziada, ambazo pia zilipatikana katika nyumba binafsi ya rais.

Baada ya uchunguzi wa awali wa Wakili wa Marekani John Lausch, Garland alisema ofisi yake iliamua kwamba wakili maalum alihitajika kuchunguza jinsi Biden alivyoshughulikia faili hizo kutokana na hali isiyo ya kawaida ya suala hilo.


"Uteuzi huu unasisitiza kwa umma kujitolea kwa idara kwa uhuru na uwajibikaji katika masuala nyeti, na kufanya maamuzi bila utata yanayoongozwa na ukweli na sheria pekee," alisema Garland.

Hur alisema atachunguza suala hilo kwa hukumu ya haki, isiyo na upendeleo.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KIAPO CHA KUKANA MAJINA



Mimi **BGUMA HALIMESHI LEOPOLD** wa kata ya Kabanga, Wilaya ya Ngara mkoa wa Kagera, mtu mzima, Mkristu, ambaye picha yangu imebandikwa juu, ninaapa na kuthibitisha yafuatayi;

1. Kwamba, Mimi nilizaliwa tarehe **03/03/1957** katika wilaya ya Ngara, mkoa wa Kagera.
2. Kwamba, jina la **BGUMA LEOPOLD HALIMESHI** ni jina langu ambalo limekosewa.
3. Kwamba, ifahamike kuwa kuanzia leo hii sitatumia jina la **BGUMA LEOPOLD HALIMESHI** na badala yake katika shughuli zangu zote nitatumia jina la **BGUMA HALIMESHI LEOPOLD.**
4. Kwamba, nimefanya kiapo hiki nikiwa na akili timamu pasipo kulazimishwa na mtu yeyote, na kwa kuzingatia **KANUNI YA VIAPO 1966.**

................................................

**Sahihi ya Muapaji**

Kiapo hiki kimefanywa na **BGUMA HALIMESHI LEOPOLD** leo hii tarehe 05/01/2023

Mbele yangu;

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1168 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late JIMMY WILFRED SAMBA**
**and**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by FRIDA SIFAEL MASUKI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **18TH day of January, 2023.**

**Dated at DAR ES SALAAM this 21st day of December, 2022.**

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NICHOLAS BENEDICT SHAYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 865 DEK – TOYOTA PASSO. Chassis namba KGC100191106. Engine namba 1KR0537693.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/OST/RB/18065/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED JUMA MKWAMA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya T**OYOTA HILUX** yenye namba za usajili **T870 DSF** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu au kupiga simu namba **0714956364** **DSM/PHQ/RB/16340/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**IBRAHIM PROTASI MREMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 194 CVR.** Chassis namba **ID3PCK6J2M2004042.** Engine namba **SRI62FMJ21004042.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/17329/2023.**

## NOTISI/ TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART & GENERAL BROKERS** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **VICTORIA FINANCE PLC,NMB BANK,AKIBA COMMERCIAL BANK** na **BRAC** ,tunatoa notisi ya kulipa madeni kwenye taasisi zote nne kwa mdaiwa hapo chini ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara kama ratiba inavyoonesha kwenye jedwali.

| SNo. | Jina la Mdaiwa | Jina la mdhamini | Dhamana | Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ROSEMARY ALOYCE MOSHA | ROSEMARY ALOYCE MOSHA | Nyumba | KIMARA TEMBONI MTAA WA MJIMPYA-UBUNGO | 31/01/2023 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishalipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0788411524/0714939933.**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MICHAEL BOAY TSAYRA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 579 APR - FUSO LORI.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: MAN/BAB/RB/9696/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 17/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MAIMUNA WA MZEE PAZI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AMADI MZEE PAZI**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **13 Mwezi wa 02 Mwaka 2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 05 Mwezi wa 01 Mwaka 2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**WU ZHOU** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 989 CDT.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/8156/2023.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NA 265 YA MWAKA 2022.**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**WILBRUGA MICHAEL PISA**
**DEOGRATIAS MICHAEL PISA................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 27 mwezi wa Machi, 2023 saa 6:00 mchana. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. Jaji Asina. A. Omari.

Imesaniniwa Dar es salaam, leo tarehe 19 mwezi wa Disemba, 2022.

## TAARIFA YA MNADA WA HADHARA

**LEGENDS AUCTION MART & GENERAL BROKERS** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED (AFCL),** tunatoa notisi ya kulipa madeni yote ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara wa kuuza dhamana zao za magari siku ya tarehe 30/01/2023 yaliyopo Vingunguti –Dar es –Salaam na SINAI-Mabatini Mwanza kuanzia Saa Tano (5:00) kamili asubuhi na kuendelea.

**ORODHA YA MALI ZITAKAZOUZWA NI KAMA IFUATAVYO HAPA CHINI**

| S/N | JINA LA MTEJA | MODEL | USAJILI | MAHALI LILIPO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SAMWEL KISAKA MZAVA | LPK 2519 | T598DMK | MWANZA |
| 2 | JULIUS GAMBA MUGETA | LPT709 | T548DXP | MWANZA |
| 3 | SASN AUTO GARAGE COMPANY LIMITED | NOVUS 340HP | T275DVM | DAR ES SALAAM |
| 4 | ISAYA LWIDIKO SANGA | LP909Bus | T424DNM | DAR ES SALAAM |
| 5 | YAMIN MOHAMED SULEIMAN | UTRA BUS | T728DVN | DAR ES SALAAM |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 na ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa
3. Gharama ya kukagua na kuona magari ni ya mnunuzi pamoja na kuhamisha umiliki ni ya mnunuzi.
4. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote akatayejaribu kuharibu mnada huu
5. Kwa mawasiliano zaidi piga namba **0714939933 AU 0788411524**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa kiburi baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# Mtake Msitake-14

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Hakuna yeyote kati ya Usonzo au Mary aliyeeleza mbele ya wanakijiji kuwa mpango wao pale ni kumuondoa, kumpeleka kwenye Hospitali ya taifa ya Muhimbili na kumtelekeza huko.

"Kila mtu anajua nini kimetokea kwenye kijiji hiki, mimi nimemuachia Mungu, na leo hii nawaaga, naondoka. Lakini kabla ya kupata madhila haya nilikuwa kwenye wakati mzuri. Na hata sasa naondoka nimekuwa na marafiki wengi hapa. Hata aliyefanya hivi pia mpaka sasa ni rafiki yangu. Imetokea tu, ajali siku zote haina kinga..."

Wakati anaongea huku baadhi ya watu waliokuwa wanamkubali na kumpenda Adel kutokana na tabia yake njema tangu alivyoingia hadi alipopofuliwa macho kwa kumwagiwa tindikali wakiwa wanamshanguilia, kulisikika muungurumo wa gari kwa mbali.

Pamoja na kwamba kulikuwa na disco linapigwa, lakini bado muungurumo ulikuwa mkubwa zaidi kila muda unavyozidi.

Na kweli, yalionekana magari matatu, Land Cruiser VX moja, V8 moja na Land Rover moja aina ya Defender nyeupe, zote zilikuwa kasi zikielekea sehemu ambayo kuna sherehe.

Baadhi waliogopa, lakini kwa sababu wengi wao walikuwa wamelewa, waliona ni jambo la kawaida. Jinsi yalivyokuwa yakikaribia vumbi lilitimka isivyo kawaida. Hakuna aliyejua ni kitu gani kimetokea.

Yalifika na kusisimama pale pale kwenye uwanja wa shule ya msingi ambapo hafla hiyo ilikuwa inafanyika. Kwa namna ambayo haikutegemewa, walishuka watu wawili tu kwenye gari VX, waliokuwa wamevaa suti zenye rangi ya bluu. Na hata hivyo bado kuna watu wengine waliokuwa wamebaki kwenye gari hilo. Hakuna yeyote aliyeshuka kwenye magari mawili yaliyobaki licha ya kwamba ndani kulikuwa na watu. Hawakuonekana ni watu wa kawaida. Ilionekana kabisa kuna jambo wamelifuata. Kuna kitu kimetokea au kinataka kutokea.

Walipofika kwenye eneo la tukio, waligawana. Mmoja alikwenda kwenye jukwaa kuu. Mwingine akaenda kwa DJ, kule ambako kuna muziki na kipaza sauti.

Yule aliyekwenda jukwaa kuu alionekana kuinama kwa Mwenyekiti wa Kijiji na kuzungumza naye.

Muda huo huo walishuka watu wengine wanne kutoka kwenye Land Rover Defender. Hawa hawakuvaa suti. Kila mmoja alivaa nguo yake anayoijua yeye. Nao walitembea taratibu kusogea kwenye sherehe ile. Vile vile nao waligawana. Wawili walisogea karibu na jukwaa kuu. Hawakufika, walisimama mbali kama watu wanaowalinda wale waliokaa hapo.

**"Wananchi wa Kijiji hiki hamjambo." Ilisikika sauti iliyosalimia kwa nguvu na bashasha. Iliposikika tu, wanakijiji wote waliondoa woga. Haikuonekana kama ni ya watu ambao ni washari, ila labda kuna kitu wanataka kueleza.**

Waliobaki wawili walionekana nao wamegawana mmoja akienda mbele zaidi na mwingine nyuma.

Ghafla muziki ulizimwa. Wengi walianza kuingiwa na hofu. Lakini kwa sababu wengi wao walikuwa wameshautwika, hofu ilikuwa inaingia na kutoka. Hakukuonekana mtu ameondoka baada ya kuona hali isiyo ya kawaida.

"Wananchi wa Kijiji hiki hamjambo." Ilisikika sauti iliyosalimia kwa nguvu na bashasha. Iliposikika tu, wanakijiji wote waliondoa woga. Haikuonekana kama ni ya watu ambao ni washari, ila labda kuna kitu wanataka kueleza.

Aliyekuwa akiwasalimia wananchi wa kijiji hicho ni yule jamaa aliyevaa suti na kwenda alipo DJ na kipaza sauti.

Baada ya kuongea kwa sekunde kadhaa na MC na DJ wake, alipewa kipaza sauti kwa ajili ya kuwasalimia watu.

"Hatujambo." Wakaitikia kwa nguvu huku wakijua kuna usalama kwani hakuonekana kama amekasirika na hata sauti haikuonekana kama ni adui.

"Nchi yetu inahitaji vitu vinne. Watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora, siyo?" Akauliza tena.

"Ndiyooo." Safari hii akaitikiwa kwa nguvu zaidi.

"Hapa kwenu watu wapo?"

"Wapooo"

"Ardhi?"

Kulikuwa na mkanganyiko kwenye kuitikia, wengine walisema ipo na wengine haipo.

"Najua siasa safi ipo kwa viongozi wenu wa juu, lakini hapa nauliza kuna uongozi bora?"

"Hakuna baba." Akajibiwa kiasi cha kumfanya jamaa aliyekuwa akiuliza kutabasamu.

"Samahani sana kwa kuingilia sijui pati, hafla ya sherehe yenu, lakini sisi ni wageni wenu baadhi wametoka mkoani na wengine Dar es Salaam, tumekuja hapa kwa ajili ya kutetea maslahi ya taifa, kijiji chenu na wanakijiji kwa ujumla."

Kuna baadhi ya watu walianza kushangilia kwa nguvu bila kujua ni kitu gani kinataka kuongelewa.

"Tumekuja kuwaokoa wananchi wa kijiji hiki kutoka kwa watu madhalimu. Kuna watu mmewapa madaraka, lakini badala ya kuwasaidia na kuwalinda, wamewafanya kuwa watumwa."

Mpaka hapo tu, tayari wanakijiji ambao ni watoto wa mjini wanasema 'waliosomea Cuba' walishaanza kuelewa kuwa hao watu walio hapo ni wa aina gani na wamekuja kufanya nini. Hivyo wakaanza kushangilia kwa nguvu.

Wale wenzangu na mimi kwenye vichwa vigumu wakaendelea kupatwa na mshangao wasielewe nini kinaendelea na kinachofanyika.

"Wananchi tumekuja hapa kuwarudishia tena kijiji kiwe mikononi mwenu na siyo mikononi mwa wakoloni weusi ambao wamewafanya watumwa. Tumepata habari kuwa hivi sasa mmekuwa watumwa ndani ya nchi yenu ya Tanzania, na kijiji chenu hiki..."

Sasa hapo kila mmoja alijua sababu ya watu wale kuja pale. Ni kuwarudishia ardhi ambayo ilichukuliwa na mwekezaji zaidi ya asilimia 70 na wao kubaki na asilimia 30 tu.

Wakajikuta badala ya kuimba nyimbo zao za disco walizokuwa wakiimba awali, wakaanza kuimba 'ukombozi, umewadia, ukombozi umewadia.' Waliimba kwa zaidi ya dakika tano.

"Ahsanteni sana wanakijiji, ahsanteni sana kwa kutuelewa mapema zaidi na kutuunga mkono. Sasa naomba tueleze kile kitu ambacho tumekusanyiwa na kuletewa Makao Makuu. Kama kuna kasoro kwa sababu nyinyi wenyewe mpo hapa mtaeleza."

Umati wa wanakijiji sasa ulizidi kumiminika zaidi. Hata wale ambao hawakuja kwenye sherehe hizo kwa sababu mbalimbali, walifika baada ya kwenda kuambiwa kuwa kuna watu ambao wamekuja kijijini hapo wanaonekana kuwa wakombozi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SINGIDA BS YAENDELEA KUSAJILI MASHINE MPYA

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

KATIKA kuimarisha safu yake ya ushambuliaji, uongozi wa Singida Big Stars umekamilisha mchakato wa kumsajili nahodha wa Aduana Stars ya Ghana, Bright Adjei, kwa mkataba wa miaka miwili.

Nyota huyo ameshatua visiwani hapa kuungana na kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya kuongeza nguvu katika mchezo wa fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa jana usiku dhidi ya Mlandege FC.

Mshambuliaji huyo alliyefikisha mabao 14 katika msimu wa 2021/22 na msimu huu kabla kutua Singida Big Stars akicheza michezo saba alizifumania vyavu za wapinzani mara tano.

Nyota huyo anaungana na Meddie Kagere, Nicolas Gyan na Kazadi Kasengu katika safu hiyo ya usambuliaji.

Mwenyekiti wa Singida Big Stars, Ibrahim Mirambo, alisema wamekamilisha usajili wa wachezaji wapya kwa asilimia 90 na wote wataonekana katika mechi watakazocheza.

Mirambo alisema ujio wa Adjei utasaidia kuongeza nguvu katika safu yao ya ushambuliaji kwa ajili ya kufanya vizuri katika michezo 11 iliyosalia ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ni kweli tumefanya usajili mkubwa kuimarisha kikosi chetu, tumeona usajili wa Kazadi, Yussuph (Kagoma), Ennock Atta Agyei, Nashon Naftal na tutamtambulisha Adjei ambaye ataonekana hivi karibuni," alisema Mirambo.

Kuhusu Kazadi kuhusishwa na Yanga, Mwenyekiti huyo alisema nyota huyo ni mali yao baada ya kumsainisha mkataba wa miaka mitatu kuitumikia timu hiyo.

"Mchezaji yeyote aliyekuwapo hapa Singida Big Stars amesajiliwa, Kazadi ni mchezaji wetu ana mkataba wa miaka mitatu kama hao Yanga wanamhitaji waje mezani kununua mkataba wake au kama wanaona hatujampa mkataba basi waje kumchukua," alisema Mirambo.

Aliongeza usajili huo umefanywa kutokana na mahitaji ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Hans van Pluijm ili kuhakikisha wanakuwa imara na kufanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu iliyopo mbele yao na kumaliza katika nafasi tatu za juu kwenye msimamo.

Singida Big Stars ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi 37 sawa na Azam FC iliyoko kwenye nafasi ya tatu kutokana na kuwa na uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa.

## Oppa aongoza ufungaji SWPL

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

WAKATI Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ikiendelea kupamba moto, tayari vita ya kuwania kiatu cha dhahabu imeanza kuonekana mapema zikiwa zimechezwa mechi tano kwa kila timu kwa msimu huu wa 2022/2o23.

Katika orodha ya wanaowania tuzo hiyo, mshambuliaji na nahodha wa Simba Queens, Oppa Clement ndiye kinara wa kutikisa nyavu akiwa amefunga mabao sita.

Oppa aliifungia Simba Queens mabao yote katika ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Amani Queens huku akikosa penalti iliyotolewa katika kipindi cha pili.

Anayefuta katika orodha ya wafungaji bora ni Cynthia Musungu wa Fountain Gate Princess, Fatuma Mustapha (JKT Queens), kila mmoja amefunga mabao manne wakati wenye magoli matatu kila mmoja ni Aniela Uwimana (Yanga Princess), Winifrida Gerald (Fountain Gate Princess) na Jackline Shija wa JKT Queens.

Akizungumzia ushindani uliopo katika ligi hiyo, Oppa alisema anamshukuru Mungu kwa ushirikiano ambao anaupata kutoka kwa wachezaji wenzake.

"Kikubwa ni sapoti katika kila mchezo, ushirikiano ndio sababu ya mimi kufanya vizuri, kwa uwezo wa Mungu naamini tutatetea taji na mfungaji bora atatoka Simba Queens," Oppa alisema.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Vijana wakifanya mazoezi kwenye Uwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park jijini Dar es Salaam ili kujiandaa na mashindano mbalimbali watakayoshiriki baadaye mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Namungo, Polisi Tanzania kibaruani

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Namungo FC kinatarajia kuwakaribisha Polisi Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.

Kaimu Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, aliliambia gazeti hili jana anaamini usajili walioufanya utasaidia kuongeza ubora katika kikosi chao na hivyo watapata matokeo mazuri.

Kitambi alisema wamejipanga kuonyesha soka la ushindani na hawajakata tamaa baada ya kushindwa kufika katika ya fainali kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo fainali yake ilichezwa jana usiku.

"Mungu akipenda tunatarajia kumalizana na mshambuliaji wetu mmoja ambaye tunamsajili kabla ya dirisha dogo la usajili halijafungwa, atasaidia kuimarisha kikosi chetu," alisema Kitambi.

Aliongeza amewaandaa vizuri wachezaji wake hasa kisaikolojia ili wapambane kusaka matokeo mazuri wanapocheza kwenye uwanja wa nyumbani.

## Wanawake Dar kupitisha katiba

**Na Khadija Mngwai**

MKUTANO Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Dar es Salaam (DWFA) unatarajia kufanyika leo hapa jijini, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa DWFA, Stephania Kabumba, alisema mkutano huo utakuwa na agenda mbalimbali ikiwamo ya kupitisha Rasimu ya Katiba.

Kabumba alisema maandalizi ya mkutano huo yamekamilisha na wajumbe kutoka katika wilaya zote tano za mkoa wa Dar es Salaam wamealikwa.

Alitaja wajumbe wa mkutano huo wanatoka katika wilaya ya Kinondoni, Ilala, Ubungo, Temeke na Kigamboni.

"Tunapenda kuwaalika wajumbe wetu kuhudhuria mkutano mkuu ili tutimize malengo ya kupata katiba na baadaye kusajiliwa, kila wilaya itawakilishwa na wajumbe watatu, tunaamini mambo yatakwenda vizuri," alisema Kabumba.

## ZISIKUPITE

### MESSI ATAKIWA SAUDIA
KLABU ya Saudi Arabia Al Hilal, wapinzani wa timu mpya ya Cristiano Ronaldo ya Al Nassr, wanamtaka mshambuliaji wa Argentina mwenye umri wa miaka 35 anayechezea Paris St-Germain, Lionel Messi kwa mkataba mnono wa dola milioni 300 kwa mwaka. ***(Mundo Deportivo)***

### ARSENAL YAMTAKA VLAHOVIC
ARSENAL wamerejesha jitihada zao za kumnunua mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 22, ambaye thamani yake ni euro milioni 110. (***La Repubblica***)

### MUDRYK AKARIBIA ARSENAL
ARSENAL wamewasilisha ofa mpya kwa winga wa Shakhtar Donetsk kutoka Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 22, huku makubaliano yakikaribia ukingoni. ***(Fabrizio Romano)***

### TROSSARD AWANIA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur imeonyesha nia ya kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Leandro Trossard, mwenye umri wa miaka 28 kutoka Brighton. ***(Evening Standard)***

### SARABIA KUTUA WOLVES
KLABU ya Wolves imekubali ofa ya kumnunua kiungo wa kati wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Hispania, Pablo Sarabia, mwenye umri wa miaka 30. (AS)

### BREE ATAJWA SOUTHAMPTON
KLABU ya Southampton inaweza kumnunua beki wa kulia wa Luton Town, James Bree, mwenye umri wa miaka 25, huku wakitafuta kusajili beki mwingine wa pembeni mwezi huu. ***(Athletic)***

### RUTTER KUWEKA REKODI
DILI la Leeds United kwa mshambuliaji wa Ufaransa na Hoffenheim, Georginio Rutter, mwenye umri wa miaka 20 litakuwa na thamani karibu pauni milioni 35 ada ambayo ni rekodi ya klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

### CANCELO SOKONI ULAYA
KLABU za Hispania, Ufaransa, Ujerumani na Italia zinafuatilia hali ya beki wa pembeni wa Ureno, Joao Cancelo, mwenye umri wa miaka 28, baada ya kupoteza nafasi yake ya kuanza katika kikosi cha Manchester City. ***(Telegraph)***

### EVERTON KUSAJILI WAWILI
KLABU ya Everton inatafuta kusajili washambuliaji wapya wawili katika dirisha dogo la mwezi huu. ***(Football Insider)***

### JIMENEZ KUTUA BESIKTAS
KLABU ya Besiktas inavutiwa na mshambuliaji wa Wolves na Mexico, Raul Jimenez, mwenye umri wa miaka 31 kama mbadala wa mshambuliaji Uholanzi anayeondoka, Wout Weghorst (30), ambaye anatazamiwa kujiunga na Manchester United. ***(Fotospor)***

### CUNHA KUBAKIA WOLVES
WOLVES inakitekeleza kipengele cha kulipa paundi milioni 44.4 kufanya mkataba wa mkopo wa mshambuliaji wa Brazil, Matheus Cunha, kutoka Atletico Madrid kuwa wa kudumu. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI, MBAPPE WATAJWA KUWANIA TUZO YA FIFA

●●●Katika kinyang'anyiro hicho yupo pia straika nyota Haaland, Benzema ingawa...

**NYON, Uswisi**

LIONEL Messi na Kylian Mbappe ni miongoni mwa wachezaji waliotajwa kuwania tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka kwa Wanaume wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kwenye orodha ya nyota 14 walioteuliwa hapo juzi.

Sherehe za tuzo za FIFA zitafanyika Februari 27, mwaka huu na kuwatambua wachezaji waliofaulu kwa kiwango cha juu kuanzia mwaka 2022 katika vipengele kadhaa, huku zawadi ya Mchezaji Bora wa FIFA wa wanaume ikiwa kivutio kikuu.

Messi, ambaye alishinda tuzo ya mwaka 2019 na kushika nafasi ya pili mbele ya Robert Lewandowski mwaka 2021, anaonekana kuwa na nafasi kubwa zaidi ya kutwaa tuzo hiyo baada ya kuisaidia Argentina kubeba Kombe la Dunia mwaka 2022.

Lilikuwa ni taji la kwanza kwa Albiceleste hao tangu mwaka 1986, na Messi alichukua jukumu muhimu katika ushindi huo wakati Argentina ilipoilaza Ufaransa kwa penalti baada ya sare ya mabao 3-3 mwezi uliopita.

Messi alifunga mabao matano na kutengeneza mengine matatu na kujishindia mpira wa dhahabu, na karibu achukue kiatu cha dhahabu pia.

Mchezaji mwenzake wa Paris Saint-Germain, Mbappe alishinda tuzo ya pili kutokana na hat-trick yake dhidi ya Argentina kwenye fainali ya kushangaza, na huenda akawa mpinzani wa karibu zaidi wa Messi.

Kama haungekuwa mwaka wa Kombe la Dunia, Erling Haaland wa Manchester City angeweza kuwa na nafasi nzuri baada ya kuanza kwa maisha ya kuvutia kwenye Ligi Kuu England.

Mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or, Karim Benzema ni miongoni mwa walioteuliwa na huenda anatarajia kumaliza katika nafasi ya tatu bora baada ya kuibeba Real Madrid hadi kutwaa taji lingine la Ligi ya Mabingwa Uaya, ingawa hakucheza fainali za Kombe la Dunia.

Kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti yuko katika kinyang'anyiro cha kuwania Kocha Bora wa FIFA kwa wanaume, ingawa Lionel Scaloni wa Argentina anaweza kuwa na nafasi kubwa.

Argentina pia inawakilishwa katika kitengo cha Kipa Bora wa FIFA wa Wanaume na Emiliano Martinez kati ya watano walioteuliwa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,065,5
MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 3.72
X | 3.53
2 | 1.89
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO: COPPA ITALIA KOMBE BAYA ZAIDI ULAYA



**ROME, Italia**

KOCHA Mkuu wa AS Roma, Jose Mourinho amesema Coppa Italia ni "Kombe baya zaidi Ulaya" licha ya ushindi wa Giallorossi hao wa wa bao 1-0 dhidi ya Genoa hapo juzi.

Kikosi cha Mourinho kilikata tiketi ya kucheza robo fainali kwa ushindi huo wa Alhamisi, kwa hisani ya Paulo Dybala aliyefunga bao la dakika ya 64.

Lakini Mourinho raia wa Ureno alilaani muundo wa Coppa Italia kutokana na ushindi wa Torino wa goli 1-0 wa muda wa ziada dhidi ya AC Milan Jumatano, ambao uliwafanya kutinga hatua ya nane bora ambapo watamenyana na Fiorentina ugenini.

"Kwanza kabisa, nitasema ningependa kushinda, nilishinda mara moja, ningependa kushinda nikiwa na Roma," alisema Mourinho akiiambia Sportmediaset.

"Nadhani ni kombe baya zaidi barani Ulaya, halilindi timu ndogo.

"Nazungumzia Torino kwa mfano wanaoshinda uwanjani kwa mabingwa wa Italia Milan, basi wanatakiwa kucheza mchezo unaofuata wa mtoano wakiwa ugenini, sielewi muundo huu wa Coppa Italia.

"Tulicheza na timu ya Serie B yenye uwanja kamili, ikiwa kuna viwanja tupu lazima waelewe kwanini tumejaa na wengine hawajajaa.

"Mchezo unaofuata wa mtoano utakuwa Naples au nyumbani na Cremonese, ikiwa tutapoteza kama mwaka jana, tutapoteza, lakini tutajaribu kushinda. Kwa kikosi kama chetu, kucheza mashindano matatu pamoja ni ngumu sana."

# Arsenal yakaribia kumnasa Mudryk

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal ina karibia ya kumnunua kiungo wa Shakhtar Donetsk, Mykhaylo Mudryk, ambaye amekuwa akiwaniwani sana na klabu hiyo baada ya kushindwa kumsajili katika dirisha lililopita.

Winga huyo wa Ukraine mwenye umri wa miaka 22 amefunga mabao 10 katika mechi 18 alizoichezea Shakhtar msimu huu, na hivyo kuongeza thamani yake.

Mudryk pia amekuwa akiwaniwa na Sevilla na Chelsea, huku Washikabuduki hao wakiripotiwa walituma ofa mbili za kuhitaji huduma yake.

Arsenal wameweka mezani ofa mpya ya tatu yenye thamani ya euro milioni 70 pamoja na nyongeza ili kumnunua Mudryk, kwa mujibu wa Fabrizio Romano.

Mazungumzo yanaendelea na pande hizo mbili zinakaribia kuafikiana, huku Mudryk akichapisha emoji ya kuomba kwenye Instagram kuashiria anataka kuchukua hatua hiyo.



## HABARI MICHEZO

505,647/-

# MAGANGA ALAMBA SUPA JACKPORT BONUS MARA 2

**Na Mwandishi Wetu**

UNAWEZA usiamini, lakini waswahili wana msemo, mgaa gaa na upwa hali wali mkavu. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa, Robert Maganga, mkazi wa mtaa wa Majengo, Kahama mkoani Shinyanga.

Akizungumza katika ofisi za Sportpesa, baada ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi, Robert Maganga, alisema alianza kucheza na Sportpesa miaka mitano iliyopita.

"Mimi nimeanza kucheza na Sportpesa kuanzia mwaka 2017, baada ya kuona washindi mbali mbali wakitangazwa kwenye mitandao ya kijamii ya Twitter, Instagram na Facebook".

Akiendelea alisema hii ni mara yake ya pili, kwa yeye kushinda Jackpot bonus, kwa kiwango cha Sh. milioni tano na kuendelea.

"Leo nimerudi ofisi za Sportpesa kama mshindi wa Supa Jackpot Bonus, baada ya kuja kwa mara ya kwanza mwaka juzi (2020), niliposhinda Jackpot Bonus ya mechi 13 ambapo nilibahatika kushinda mechi 12".

Kuhusu mkeka wake ambao umeshinda alieleza aliweka Jumatatu ya kwanza ya mwaka 2023 na baada ya hapo siku ya Jumamosi alikua amepatia kwa usahihi mechi 10 kati ya mechi 17.

"Ilipofika mechi ya Spezia na Lecce, hii ilinipa presha kwa sababu ilikuwa tayari inaenda kunikosesha Sh. milioni tano katika mkeka mwingine. Baada ya hapo nilifuatilia mechi zote mpaka mwisho na kupata sms ya kunipongeza kwa ushindi wa Supa Jackpot Bonus," Maganga alisema.

Manganga alisema fedha hiyo aliyoshinda atanunua chombo cha usafiri wa bodaboda na zitakazo bakia ataangalia afanye nini katika siku za usoni.




"Napenda niwahakikishie Watanzania wenzangu mimi ndiye shuhuda ambaye mara mbili sasa nashinda kupitia Jackpot Bonus. Sportpesa wanatoa pesa kwa wakati na hakuna longolongo,"aliongeza.

Naye Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Maganga na kumtaka aendelee na mwendo huo huo wa kucheza.

"Nafikiri Watanzania wanaweza kujionea wenyewe, wewe ndio umefungua pazia la washindi la kwa mwaka 2023. Nikuombe ukazie hapo hapo usije ukaachia, kwani kuna siku utaweza kuchomoka na Jackpot ya mechi 17 inayoanzia bilioni moja na uinuke kiuchumi kama ambavyo umeweza kushinda Jackpot bonus mara mbili".

Wiki hii Supa Jackpot imesimamia 1,065,505,647.

# IHEFU YAIREJESHA

INATOKA UK. 24

wapya katika mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Ihefu siku ya Jumatatu. Mechi hiyo ni mechi ya kisasi, tujitokeze kwa wingi tuonyeshe hasira zetu kwa kuwafunga mabao mengi, tunataka kuonyesha jinsi gani tuliumia kwa kipigo kile kilichosababisha tushindwe kufikisha Unbeaten ya 50," alisema Kamwe.

Naye Kocha Msaidizi wa Ihefu, Zuberi Katwila, alisema kikosi chao kambini kwa ajili ya kujiandaa na raundi inayofuata ya ligi hiyo na sio Yanga pekee.

Katwila alisema Ihefu wanajimarisha kuona wanashinda mechi zote zilizo mbele yao na kamwe hawafanyi maandalizi kwa kuitazama Yanga peke yake.

"Ni mechi ngumu kwetu, hatuwezi kuangalia kile tulichokipiga katika mchezo wa kwanza, tutaingia uwanjani na mbinu tofauti sababu, kila mchezo unakuwa na maandalizi yake. Tunapambania alama tatu kama ilivyo kwa Yanga ambao inahitaji kuendelea kuongoza, upande wetu tunahitaji kukaa nafasi nzuri zaidi ya hapa tulipo sasa," alisema Katwila.

Ihefu imejiimarisha kwa kumsajili straika, Adam Adam na beki wa zamani wa Azam FC, David Mwantika

Katika hatua nyingine, Yanga itaikaribisha Rhino Rangers inayoshiriki Ligi Daraja la Pili katika mechi ya Kombe la FA itakayochezwa jijini kati ya Machi 3 hadi 5, mwaka huu ili kusaka timu 16 bora.

# Robertino ataka ufundi

INATOKA UK. 24

na mashabiki wa Simba wazidi kunisapoti, watarajie mazuri zaidi yanakuja," alisema nyota huyo.

Wakati huo huo, Simba imepangwa kukutana na Coastal Union katika mechi ya Kombe la FA wakati Azam FC ikitarajiwa kuwavaa Dodoma Jiji kati ya Machi 3 hadi 5, mwaka huu hapa jijini.

Kwa mujibu wa droo iliyochezeshwa jana, Namungo itaicheza dhidi ya Ihefu, Kagera Sugar watakaribisha Ken Gold, Mtibwa Sugar watawavaa Buhaya FC, Geita Gold itacheza dhidi ya Nzega United huku Gwambina itakuwa nyumbani dhidi ya Pan African.

Mashujaa wao watacheza dhidi ya Prisons na kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya kutakuwa na 'dabi' kati ya Mbeya Kwanza dhidi ya Mbeya City wakati KMC itawaalika Copco, Polisi Tanzania vs JKT Tanzania, Mapinduzi vs Polisi Katavi, Green Warriors vs Mbuni na New Dunde itawaalika African Sports.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/01/23 | 18:00 | Nottingham Forest vs Leicester City | 2.80 | 3.30 | 2.46 |
| 02. 14/01/23 | 18:00 | Wolverhampton Wanderers vs West Ham United | 2.65 | 3.20 | 2.65 |
| 03. 14/01/23 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich Albion | 2.95 | 3.20 | 2.40 |
| 04. 14/01/23 | 18:00 | Preston North End vs Norwich City | 2.95 | 3.25 | 2.38 |
| 05. 14/01/23 | 18:00 | Reading FC vs Queens Park Rangers | 2.46 | 3.25 | 2.80 |
| 06. 14/01/23 | 18:00 | Sunderland AFC vs Swansea City | 2.49 | 3.25 | 2.75 |
| 07. 14/01/23 | 18:00 | DR Congo vs Uganda | 2.39 | 2.75 | 3.45 |
| 08. 14/01/23 | 18:15 | Girona FC vs Sevilla FC | 2.40 | 3.25 | 2.90 |
| 09. 14/01/23 | 20:15 | KAS Eupen vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.35 | 2.42 |
| 10. 14/01/23 | 20:45 | FC Volendam vs RKC Waalwijk | 2.65 | 3.50 | 2.46 |
| 11. 14/01/23 | 21:00 | Ivory Coast vs Senegal | 2.85 | 2.95 | 2.65 |
| 12. 14/01/23 | 23:00 | Real Sociedad San Sebastian vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.15 | 2.80 |
| 13. 15/01/23 | 16:00 | Getafe CF vs Espanyol Barcelona | 2.50 | 2.95 | 2.95 |
| 14. 15/01/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs FC Utrecht | 2.80 | 3.50 | 2.35 |
| 15. 15/01/23 | 17:00 | Angers SCO vs Clermont Foot 63 | 2.42 | 3.40 | 2.75 |
| 16. 15/01/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs FC Nantes | 2.45 | 3.40 | 2.70 |
| 17. 15/01/23 | 17:00 | Stade Reims vs OGC Nice | 2.55 | 3.20 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 14/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 2265 | Manchester Utd vs Manchester City | 3.72 | 3.53 | 1.89 |
| 15:30 | 4530 | Rotherham vs Blackburn | 3.18 | 3.32 | 2.15 |
| 16:00 | 3730 | Geita Gold FC vs Dodoma FC | 1.99 | 3.01 | 3.78 |
| 16:00 | 4754 | Valladolid vs Rayo Vallecano | 2.69 | 3.19 | 2.59 |
| 16:30 | 2953 | Orlando Pirates vs Golden Arrows | 1.83 | 3.27 | 4.36 |
| 16:30 | 3282 | Marumo Gallants FC vs Richards Bay FC | 2.63 | 2.78 | 2.93 |
| 17:00 | 2863 | Cremonese vs Monza | 2.77 | 3.21 | 2.45 |
| 18:00 | 1550 | Bolton vs Portsmouth | 2.06 | 3.37 | 3.37 |
| 18:00 | 2368 | Wolverhampton vs West Ham | 2.59 | 3.18 | 2.64 |
| 18:00 | 2643 | Carlisle vs Newport | 2.11 | 3.18 | 3.42 |
| 18:00 | 2737 | Nottingham vs Leicester | 2.62 | 3.22 | 2.58 |
| 18:00 | 3185 | Reading vs QPR | 2.61 | 3.11 | 2.66 |
| 18:00 | 3595 | Luton Town vs West Bromwich | 2.92 | 3.16 | 2.37 |
| 18:00 | 3854 | Swindon Town vs Grimsby | 2.40 | 3.12 | 2.92 |
| 18:00 | 3997 | St Johnstone vs Livingston | 2.39 | 3.04 | 3.04 |
| 18:00 | 4233 | Hibernian vs Dundee Utd | 1.68 | 3.68 | 4.78 |
| 18:00 | 4279 | Brighton vs Liverpool | 3.12 | 3.56 | 2.09 |
| 18:00 | 4280 | Sunderland vs Swansea | 2.53 | 3.22 | 2.68 |
| 18:00 | 4575 | Everton vs Southampton | 2.20 | 3.22 | 3.17 |
| 18:00 | 4986 | Middlesbrough vs Millwall | 1.93 | 3.37 | 3.77 |
| 18:00 | 5089 | Sheffield Utd vs Stoke City | 1.71 | 3.61 | 4.55 |
| 18:00 | 5224 | Bristol City vs Birmingham | 2.23 | 3.22 | 3.12 |
| 18:00 | 5520 | Cardiff vs Wigan | 1.95 | 3.32 | 3.76 |
| 18:00 | 5538 | Hamilton vs Morton | 2.77 | 3.17 | 2.45 |
| 18:00 | 5545 | Lamia vs Atromitos | 2.54 | 2.99 | 2.89 |
| 18:00 | 5813 | MK Dons vs Lincoln | 2.04 | 3.28 | 3.53 |
| 18:00 | 5888 | Watford vs Blackpool | 1.77 | 3.62 | 4.16 |
| 18:15 | 4942 | Girona vs Sevilla FC | 2.42 | 3.26 | 2.86 |
| 18:30 | 2440 | Chippa Utd vs Cape Town City | 3.05 | 3.10 | 2.39 |
| 18:30 | 5526 | Stellenbosch vs Sekhukhune United | 2.22 | 2.89 | 3.53 |
| 19:00 | 1218 | Lens vs AJ Auxerre | 1.33 | 4.89 | 8.58 |
| 19:00 | 5537 | Namungo vs Polisi Tanzania | 1.87 | 3.20 | 4.50 |
| 20:00 | 2119 | Maccabi Netanya vs Hapoel Haifa | 1.85 | 3.41 | 3.75 |
| 20:00 | 5630 | Lecce vs AC Milan | 5.53 | 3.80 | 1.57 |
| 20:30 | 3725 | Osasuna vs Mallorca | 2.02 | 3.09 | 3.99 |
| 20:30 | 3752 | Bnei Sakhnin vs Hapoel Beer Sheva | 4.47 | 3.79 | 1.63 |
| 20:30 | 3977 | Brentford vs Bournemouth | 1.62 | 3.92 | 4.86 |
| 20:30 | 5825 | Racing Santander vs Sporting Gijon | 2.53 | 2.83 | 3.02 |
| 20:45 | 4473 | FC Volendam vs Waalwick | 2.53 | 3.37 | 2.58 |
| 20:45 | 5716 | Heerenveen vs AZ Alkmaar | 3.17 | 3.37 | 2.14 |
| 21:00 | 2108 | Rio Ave vs Pacos Ferreira | 1.91 | 3.33 | 3.98 |
| 21:00 | 3636 | Marseille vs Lorient | 1.38 | 4.78 | 6.97 |
| 21:00 | 4453 | PAOK vs OFI Crete | 1.36 | 4.38 | 8.77 |
| 22:45 | 5425 | Inter vs Verona | 1.28 | 5.55 | 8.52 |
| 23:00 | 2339 | Ajax vs Twente | 1.32 | 5.33 | 7.31 |
| 23:00 | 2486 | Sparta Rotterdam vs SBV Excelsior | 1.50 | 4.26 | 5.54 |
| 23:00 | 4451 | Levante vs Granada | 2.10 | 3.07 | 3.61 |
| 23:00 | 5094 | Real Sociedad vs Athletic Bilbao | 2.44 | 3.11 | 2.96 |
| 23:00 | 5568 | Lyon vs Strasbourg | 1.58 | 4.06 | 5.15 |
| 23:30 | 2541 | Sporting Braga vs Boavista | 1.30 | 5.16 | 8.93 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Januari 14, 2023
Nipashe




UKURASA 21

## Messi, Mbappe watajwa kuwania tuzo ya FIFA



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (aliyeruka juu), akiwania mpira katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Al Dhafra ya Falme za Kiarabu iliyochezwa kwenye mji wa Abu Dhabi jana. Simba ilifungwa bao 1-0. **PICHA: SIMBA SC**

# IHEFU YAIREJESHA YANGA DARASANI

## Jangwani yapania kulipiza kisasi, yapangwa na Rhino Rangers katika...

**Na Saada Akida, ZANZIBAR**

WAKATI Yanga wakitumia mchezo dhidi ya Ihefu SC kutambulisha wachezaji wapya, iliyowasajili, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Cedric Kaze, ameanza kuisuka upya safu ya ulinzi na kuwaboresha washambuliaji kwa lengo la kumaliza hasira dhidi ya wapinzani wao hao kutoka Mbarali, Mbeya.

Yanga itaikaribisha Ihefu katika mechi ya raundi ya 20 ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kichapo cha mabao 2-1 walichopata Novemba 28, mwaka jana, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Highland Estates.

Hata hivyo, katika mechi hiyo Yanga itawakosa nyota wake ambao ni Stephen Azizi Ki, Bernard Morrison, Djigui Diara, Khalid Aucho, Djuma Shaban, Yannick Bangala na Joyce Lomalisa huku Kocha Mkuu, Nesreddine Nabi, akirejea nchini jana akitokea kwao Tunisia alipokwenda katika mapumziko mafupi.

Kaze aliliambia gazeti hili anataka kuona safu yake ya ulinzi inaongeza umakini kwa kucheza kwa tahadhari wakati wote wa mchezo huo.

Kocha huyo alisema pia anataka kuona washambuliaji wake wakiongozwa na kinara wa mabao, Fiston Mayele, wanatumia vyema kila nafasi watakayotengeneza ili kupata ushindi mnono wa mabao katika mechi hiyo na kujiimarisha kileleni.

Alisema anatambua mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu wanahitaji kupata pointi tatu muhimu huku Ihefu nao wakidhamiria kuonyesha ubabe.

Aliongeza wanafanya kazi kubwa katika kuondoa au kupunguza madhaifu waliyonayo ili wapate matokeo chanya na hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea katika msimu huu.

"Tumerejea kambini kujiandaa na mechi dhidi ya Ihefu, tulipoteza mechi ya kwanza na sasa hatutaki kurudia makosa ya awali, tunahitaji ushindi wa mabao mengi na pia kutoruhusu wapinzani wetu kufika golini au kuruhusu bao.

Kazi kubwa ya mabeki ni kuongeza umakini kwa kuwachunga wapinzani, pamoja na safu yetu ya ushambuliaji kuhakikisha inatumia vizuri nafasi wanazotengeneza ili kutafuta ushindi," alisema Kaze.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema mechi hiyo ni maalum kwa ajili ya kutambulisha wachezaji wao wapya ambao wamesajiliwa dirisha dogo linalotarajiwa kufungwa hapo kesho.

"Tutawambulisha wachezaji wetu wote

INAENDELEA UK. 23

## Robertino ataka ufundi, burudani

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba Roberto Oliveria amewaambia wachezaji anataka mpira uchezwe zaidi kwenye eneo la wapinzani wao na si kwao, huku akianzisha mazoezi maalum kwa ajili ya wanaocheza katika safu ya mbele tu.

Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza, alisema hayo katika mahojiano maalum jijini, Abu Dhabu, Falme za Kiarabu walikoweka kambi ya muda mfupi.

Ntibazonkiza aliyesajiliwa na Simba kipindi hiki cha dirisha dogo, alisema Robertinho ameegemea zaidi katika eneo la ushambuliaji na hata baada ya mazoezi ya timu nzima, bado anakuwa tena na programu maalum ya ziada kwa ajili ya kufundisha namna ya kushambulia ambayo anawapata mastraika, mawinga na viungo washambuliaji.

"Mazoezi yanakwenda vizuri na wachezaji tupo vizuri majeruhi wameshaanza kurejea, kweli kocha mkuu kuna kitu amekibadilisha, kwa wachezaji tunafurahia mazoezi na kuna kitu anachotuongezea, hasa upande wa ushambuliaji tunaona kuna kitu kikubwa anatupa," alisema mchezaji huyo raia ya Burundi.

Alisema kwa aina ya mazoezi wanayofanya, ana imani siku zinavyozidi kusonga mbele, eneo la ushambuliaji la timu yao litakuwa limebadilika kwa kiasi kikubwa.

"Alivyofika tu na kuanza mazoezi, alituambia tuchezee sana upande wa mpinzani, ndiyo maana amekuwa akitukomalia sana sehemu ya mbele na hata baada ya mazoezi huwa na mazoezi mengine maalum kwa wachezaji wanaocheza nafasi ya mbele, ametusaidia na tukiendelea hivi naona mstari wa mbele utakuwa hatari sana," alisema Ntibazonkiza.

Nyota huyo pia alionyesha kufurahishwa jinsi alivyopokewa na wanachama na mashabiki wa timu hiyo, huku akimpongeza shabiki mmoja aliyeweka picha yake kubwa kwenye bajaji na kuandika 'kumbe siyo mzee.'

Picha ya bajaj hiyo ameonekana kuvutia wengi kwenye mitandao ya kijamii, huku mwenyewe akisema ameiona.

"Nimeiona ile bajaj, nilicheka sana, na bado Mwenyezi Mungu ndiyo hakimu. Sikutarajiwa vile ila nashukuru kuona kuna mashabiki wananisapoti, wananikumbali, naomba wanachama

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >